


# Hazelwood School District



*"A Culture of High Expectations and Excellence!"*


**SHULE YA WILAYA YA HAZELWOOD**

*Utamaduni wa Matarajio Makubwa na Ubora!*

**2020-2021**

**MWANAFUNZI-MZAZI**

**KIJITABU CHA MAELEKEZO / MWONGOZO WA  
TABIA**

Hazelwood  
School   
District

*"A Culture of High Expectations and Excellence!"*

## FAHARASA

### UTANGULIZI

|   |   |
|---|---|
| <b>BODI YA ELIMU</b>                        | 1 |
| <b>BARUA YA KUWAKARIBISHA TENA SHULENI</b>  | 2 |
| <b>TAARIFA ZA DHAMIRA, MAONO NA THAMANI</b> | 3 |

### KIJITABU CHA MAELEZO

|  |        |
|--|--------|
| <b>MAHUDHURIO</b>  | 4      |
| - KUTOKUWEPO   | 4      |
| <b>TARATIBU ZA MAHUDHURIO</b>                            | 5      |
| - SIMU YA KUTOKUWEPO                                     | 5      |
| - KURUHUSIWA KUONDOKA                                    | 5      |
| - MASAA  | 6      |
| - KUWASILI KUCHELEWA                                     | 6      |
| - KAZI YA MUDA ULIOPOTEA                                 | 6      |
| - KUCHELEWA  | 6      |
| <b>MAHITAJI YA MAHUDHURIO NA KURIPOTI</b>                | 6      |
| - MASUALA YA KISHERIA                                    | 6      |
| - MAWASILIANO  | 6      |
| - MAJUKUMU YA SHULE                                      | 6      |
| - MAJUKUMU YA MWALIMU                                    | 7      |
| - MAJUKUMU YA MZAZI/MLEZI                                | 7      |
| - MAJUKUMU YA MWANAFUNZI                                 | 8      |
| <b>PROGRAMU ZA A+ ZA SHULE (SHULE YA SEKONDARI)</b>      | 8      |
| <b>UTUNZAJI KABLA NA BAADA YA SHULE</b>                  | 8      |
| <b>UONEVU/UNYANYASAJI</b>                                | 9 – 12 |
| <b>MKAHAWA NA HUDUMA ZA CHAKULA</b>                      | 12     |
| - SHULE YA MSINGI  | 13     |
| - SHULE YA KATI / YA SEKONDARI                           | 13     |
| <b>UNYANYASAJI NA KUTOTUNZA WATOTO</b>                   | 13     |
| <b>URAI NA ADHABU</b>                                    | 13     |
| - USHIRIKI WA RIADHA NA MWENENDO KATIKA TUKIO            | 14     |
| <b>MAWASILIANO NA KUTEMBELEA SHULE</b>                   | 14     |
| - BODI YA ELIMU  | 14     |
| - MABADILIKO YA ANWANI AU NAMBA YA SIMU                  | 14     |
| - KUWASILIANA NA WALIMU                                  | 14     |
| - MAWASILIANO YA KITIVO/WAFANYAKAZI                      | 14     |
| - MIKUTANO YA WAZAZI                                     | 15     |
| - KITUO CHA WAZAZI MTANDAONI                             | 15     |
| - MATEMBEZI YA WAZAZI                                    | 15     |
| - KADI ZA RIPOTI NA RIPOTI ZA MAENDELEO                  | 15     |
| - SHULE KUFUNGUA KWA AJILI YA HEWA MBAYA—953-THELUJI     | 16     |
| - MAWASILIANO YA SHULE-NA-NYUMBANI                       | 16     |
| - SIMU NA UJUMBE   | 16     |
| <b>MAHITAJI YA HUDUMA YA JAMII (SHULE ZA SEKONDARI)</b>  | 16     |
| <b>MTAALA, KUWEKA ALAMA NA KAZI YA KUFANYIA NYUMBANI</b> | 16     |
| - VIWANGO VYA KITAALUMA NA MIZANI YA KUWEKA ALAMA        | 17     |
| <b>SHULE YA MSINGI</b>                                   | 17     |
| - MIZANI YA KUWEKA ALAMA                                 | 17     |
| - TARATIBU ZA KUWEKA ALAMA                               | 17     |
| <b>SHULE YA KATI</b>                                     | 17     |
| - MIZANI YA KUWEKA ALAMA                                 | 18     |
| - TARATIBU ZA KUWEKA ALAMA                               | 18     |
| <b>SHULE YA SEKONDARI</b>                                | 18     |
| - MIZANI YA KUWEKA ALAMA                                 | 18     |
| - TARATIBU ZA KUWEKA ALAMA - TATHMINI (MITIHANI)         | 18     |
| - TARATIBU ZA KUWEKA ALAMA ZA MARUDIO “BADO”             | 19     |
| - KAZI YA KUFANYIA NYUMBANI                              | 20     |
| - MIONGOZO YA JUMLA YA KAZI YA KUFANYIA NYUMBANI         | 20     |
| - MAJUKUMU YA MWALIMU                                    | 21     |
| - MAJUKUMU YA MZAZI                                      | 21     |
| - MAJUKUMU YA MWANAFUNZI                                 | 22     |
| - MIONGOZO YA KAZI YA KUFANYIA NYUMBANI KUCHELEWA        | 22     |


|  |                |
|--|----------------|
| <b>KANUNI YA MAVAZI</b>  | <b>22</b>      |
| - SARE ZA SHULE  | 22             |
| <b>KUFUNGWA KWA DHARURA NA KURUHUSIWA KUONDOKA MAPEMA</b>              | <b>23</b>      |
| - KURUHUSIWA KUONDOKA MAPEMA KUTOKANA NA DHARURA                       | 23             |
| - MAWASILIANO YA DHARURA   | 23             |
| <b>MAZOEZI ZA WAKATI WA DHARURA</b>                                    | <b>23</b>      |
| <b>SAFARI ZA MASOMO YA NJE</b>   | <b>23</b>      |
| <b>MAELEKO NA HUDUMA ZA MWONGOZO NA USHAURI</b>                        | <b>23</b>      |
| <b>PASI ZA UKUMBINI</b>  | <b>24</b>      |
| <b>UNYANYASAJI</b>   | <b>24</b>      |
| <b>AFYA NA USALAMA</b>   | <b>24</b>      |
| - MAGONJWA YA KUAMBUKIZA   | 24             |
| - VIGEZO VYA KUTENGWA SHULENI (KUDHIBITI MAGONJWA YA KUAMBUKIZA)       | 24             |
| - DAWA ZA DHARURA  | 25             |
| - KUSAMEHEWA KUTOKA KWA ELIMU YA MAZOEZI AU SHUGHULI ZA NJE            | 25             |
| - KUFUNZWA NYUMBANI KUTOKANA NA UGONJWA WA MUDA MREFU                  | 25             |
| - UGONJWA AU MAJERAHA  | 25             |
| - CHANJO   | 26             |
| - TAARIFA ZA MATIBABU  | 26             |
| - TATHMINI YA AFYA YA AKILI NA HUDUMA ZA USHAURI NASAHA                | 26             |
| - UCHUNGUZI WA KIMWILI   | 26             |
| - TARATIBU ZA KUSIMAMIA DAWA ZA WANAFUNZI WANA OHITAJI DAWA SHULENI    | 27             |
| - MAHITAJI MAALUM YA MATIBABU  | 27             |
| <b>SERA YA KITAMBULISHO (SHULE ZA KATI NA SEKONDARI TU)</b>            | <b>28</b>      |
| <b>IKIWA KUNA SUALA SHULENI</b>  | <b>28</b>      |
| <b>MATUMIZI YA MTANDAO</b>   | <b>28</b>      |
| <b>KUONDOKA CHUONI</b>   | <b>29</b>      |
| <b>TARATIBU YA MAKTABA</b>   | <b>29</b>      |
| <b>MAKABATI</b>  | <b>29</b>      |
| <b>TARATIBU ZA MAEGESHO (SHULE YA SEKONDARI)</b>                       | <b>29</b>      |
| <b>VITAFUNIO/VYA KUFURAHISHA VYAKARAMU(SHULE YA MSINGI)</b>            | <b>30</b>      |
| <b>MAKAZI</b>  | <b>30</b>      |
| <b>USALAMA NA AMANI</b>  | <b>31</b>      |
| - SIMU YA MOJA KWA MOJA YA SHULE SALAMA                                | 31             |
| <b>KUOMBAOMBA</b>  | <b>31</b>      |
| <b>PROGRAMU MAALUM</b>   | <b>31</b>      |
| <b>HUDUMA MAALUM ZA ELIMU HUTOLEWA</b>                                 | <b>31</b>      |
| <b>NA WAFANYAKAZI MAALUM WA WILAYA YA SHULE</b>                        | <b>31</b>      |
| <b>VITABU VYA KIADA</b>  | <b>31</b>      |
| <b>NAKALA</b>  | <b>31</b>      |
| <b>WATU WA KUJITOLEA</b>   | <b>32 – 33</b> |
| <b>USALAMA WA MATETEMEKO LA ARDHI KWA SHULE ZA MISSOURI</b>            | <b>34 – 36</b> |
| <b>NOTISI ZA UMMA</b>  | <b>37</b>      |
| <b>TARATIBU ZA ULALAMISHI</b>  | <b>38 - 39</b> |
| <b>MAFUNZO KWA WOTE - SERA YA MATUMIZI INAYOKUBALIKA YA MTANDAO</b>    | <b>40 – 42</b> |
| <b>SHERIA YA HAKI ZA ELIMU YA FAMILIA NA SHERIA YA FARAGHA (FERPA)</b> | <b>43</b>      |

## MWONGOZO WA TABIA

|  |         |
|--|---------|
| <b>UTANGULIZI</b>  | 46      |
| <b>KURIPOTI NA KURECODI ADHABU NA KUMBUKUMBU</b>   | 46      |
| - USIRI (SERA JGF)   | 47      |
| - TABIA NJE YA CHUO  | 47      |
| - KURIPOTI KWA WAFANYAKAZI WA SHULE (SERA JGF)   | 47      |
| - KUTOA TAARIFA KWA MAAFISA WA UTEKELEZAJI WA SHERIA (SERA JGF)                          | 47      |
| - UTEKELEZAJI WA SHERIA KUTOA TAARIFA KWA MRATIBU  | 48      |
| - WANAFUNZI WASIO RUHUSIWA KUHUDHURIA AU KUJIANDIKISHA                                   | 48      |
| - KUMBUKUMBU ZA ADHABU YA MWANAFUNZI (SERA JGF)  | 49      |
| - WANAFUNZI WANAPOKEA HUDUMA MAALUM YA ELIMU (SERA JGE)                                  | 49      |
| <b>HATUA CHANYA YA MIINGILIO KATI NA MISAADA YA KITABIA (PBIS)</b>                       | 50      |
| - MATARAJIO YA TABIA YA MWANAFUNZI   | 51      |
| <b>HAKI NA MAJUKUMU ZA WANAFUNZI, WAZAZI NA WAFANYAKAZI WA SHULE</b>                     | 51      |
| I. HAKI ZA MWANAFUNZI  | 51      |
| II. MAJUKUMU YA MWANAFUNZI   | 52      |
| III. HAKI NA MAJUKUMU ZA WAZAZI/WALEZI   | 52      |
| IV. HAKI NA MAJUKUMU ZA WAFANYAKAZI WA SHULE   | 53      |
| <b>MIONGOZO YA HAZELWOOD YANAANZA NA KUMALIZIKA LINI?</b>                                | 54      |
| <b>TARATIBU ZA ADHABU NA MCHAKATO UNAOSTAHILI</b>  | 55      |
| <b>UFAFANUZI WA MANENO</b>   | 56      |
| - TABIA YA KINTENDO CHA KUVURUGA/VURUGU SHULENI  | 56      |
| - KITUO CHA USAIDIZI MBADALA (ASC)   | 56      |
| - RUFANI   | 57      |
| * NGAZI YA MJENGO  | 57      |
| * NGAZI YA WILAYA  | 57      |
| - MKATABA/MPANGO YA TABIA AU MPANGO WA KUIINGILIA KATI                                   | 57      |
| - MKUTANO WA TIMU YA UTUNZAJI/ TIMU YA MSAADA WA WANAFUNZI                               | 57      |
| - KUIINGILIA NA KUTOKA NJE   | 57      |
| - UPATANISHI WA MIGOGORO (IKIELEKEZWA NA MWENZI NA/AU MTU MZIMA)                         | 57      |
| - ADHABU ZA VIBOKO (IMEPIGWA MARUFUKU) (SERA JCA)  | 57      |
| - UINGILIAJI KATI WA MSHAURI / MFANYAKAZI WA KIJAMII                                     | 58      |
| - KIZUIZINI  | 58      |
| - KUSIKILIZWA KWA ADHABU (DH)  | 58      |
| - TATHMINI YA TABIA INAYOFANYA KAZI  | 58      |
| - PASI YA UKUMBINI   | 58      |
| - MWENENDO MBAYA   | 59      |
| - HAJA YA KUJUA (SERA JGF)   | 59      |
| - MKUTANO WA MZAZI   | 59      |
| - MAWASILIANI YA MZAZI   | 59      |
| - PROGRAMU YA CHAGUO CHANYA (PC)   | 59      |
| - RUFAA KWA SHIRIKA LA NJE   | 59      |
| - SHUGHULI YA KUTAFAKARI   | 59      |
| - MATARAJIO YA KUFUNDISHA UPYA   | 59      |
| - KUIINGILIA MWINGINE  | 59      |
| - MAFUNZO YA MGUSO SALAMA/ T-SALAMA/ VIJANA SALAMA                                       | 60      |
| - KIZUIZINI JUMAMOSI   | 60      |
| - MALI YA SHULE  | 60      |
| - AFISA WA RASILIMALI YA SHULE KUIINGILIA KATI   | 60      |
| - RUFAA/MKUTANO WA AFISA WA SHULE WA RASILIMALI  | 60      |
| - KUUZA/KUOMBAOMBA   | 60      |
| - SIEP (PROGRAMU YA KUIINGILIA KATI NA ELIMU YA POMBE NA DAWA ZA KULEVYA)                | 60      |
| - MAFUNZO YA UJUZI WA KIJAMII  | 61      |
| - BEJI ZA UTAMBULISHO WA MWANAFUNZI  | 61      |
| - KUSIMAMISHWA KWA MUDA NA KUONDOLEWA (SERA JGD)   | 61      |
| <b>ORODHA YA UINGILIAJI KATI</b>   | 62 – 63 |
| <b>MWONGOZO WA TABIA YA MWANAFUNZI, MAKOSA, MATOKEO, UINGILIAJI KATI NA MISAADA</b>      | 64      |
| - MFUMO WA VIWANGO VYA MATOKEO   | 64      |
| - UINGILIAJI KATI NA MISAADA   | 64      |
| <b>MAZOEYA YA UREJESHO</b>   | 64 - 79 |
| <b>MATARAJIO YA WILAYA YA SHULE YA HAZELWOOD KWA WATEMBEAJI WA MADARASA ZA K-12</b>      | 80      |
| <b>MATARAJIO YA WILAYA YA SHULE YA HAZELWOOD KWA WASAFIRI WA MABASI WA MADARASA K-12</b> | 80 – 81 |
| - SIMU YA MOJA KWA MOJA YA SHULE SALAMA  | 82      |
| <b>WASIMAMIZI WA WILAYA YA SHULE YA HAZELWOOD</b>  | 83      |

|  |         |
|--|---------|
| - Shule ya Msingi  | 83      |
| - Shule ya Kati  | 84      |
| - Shule ya Sekondari   | 85      |
| <b>KAZI ZA USIMAMIZI WA MSAIDIZI WA MRATIBU</b>                      | 86      |
| <b>WANACHAMA WA KAMITI YA MWONGOZO WA TABIA ZA WANAFUNZI</b>         | 87 – 91 |
| <b>FOMU YA SAINI YA MZAZI/MLEZI NA MWANAFUNZI</b>                    | 92      |
| <b>KALENDA YA KITAALUMA YA 2021-2022</b>                             | 93      |
| <b>ZIDI KUAMBIWA NA KUUNGANISHWA NA WILAYA YA SHULE YA HAZELWOOD</b> | 94      |

# Hazelwood School District



*"A Culture of High Expectations and Excellence!"*

*Utamaduni wa Matarajio Makubwa na Ubora!*

## **KUMBUKUMBU ZA KIELIMU**

Hakuna mtu mwingine isipokuwa mzazi wa mwanafunzi au mlezi wa kisheria anayeweza kufikia kumbukumbu za elimu zaidi ya taarifa za kuorodhesha. Mwanafunzi anayestahiki (umri wa miaka 18) anaweza pia kufikia kumbukumbu zao za kielimu. Kwa hiyo, Wilaya ya Shule ya Hazelwood haiwezi, kisheria, kushiriki jinsi wanafunzi wana adhibiwa na watu wengine isipokuwa mzazi wa mwanafunzi huyo au mlezi wa kisheria.

# Hazelwood School District



*"A Culture of High Expectations and Excellence!"*  
*Utamaduni wa Matarajio Makubwa na Ubora!*

## **BODI YA ELIMU**

Cheryl D. Latham, Rais

Diane Livingston, Makamu wa Rais

Betsy Rachel, Katibu

Dk. Zella Williams, Mweka Hazina

Margo McNeil, Mkurugenzi

Dk. Brenda C. Youngblood, Mkurugenzi

## **MRAKIBU WA SHULE**

Dk. Nettie Collins-Hart





*"A Culture of High Expectations and Excellence!"  
Utamaduni wa Matarajio Makubwa na Ubora!*

Dk. Nettie Collins-Bert Mrakibu  
Bodi ya Elimu  
Cheryl Latham, MCBM  
Diane Livingston, CBM  
Betsy Rachel, CBM  
Dk. Zella Wiffiams, CBM  
Margo McNeil, CBM  
Dk., Brenda C. Youngblood,  
MQM.

Agosti 21, 2020

Wapendwa Wanafunzi, Wazazi na/au Walezi:

Karibuni kwa mwaka wa shule ya 2021-2022! Mada ya mwaka huu, "Wilaya ya Shule ya Hazelwood: Kubadilika Pamoja," inazungumzia ahadi yetu ya kukumbatia hatua mpya za usalama, mbinu za kusomesha, na fursa za kujifunza.

Tunapoingia katika mwaka mpya wa shule ya kulisimua, uelewa wetu wa pamoja wa matarajio ya wilaya nzima ni muhimu kwa mafanikio yetu. Kuwa na hayo maanani, tumeunda Kijitabu hiki cha Maelekezo ya Mwanafunzi na Mwongozo wa Tabia kwa familia yako. Ukaguzi wako kwa umakini wa kijitabu hiki utaongeza uelewaji wako na uelewaji wa matarajio ya Wilaya ya Shule ya Hazelwood, rasilimali, misaada, na michakato

Nina, tazamia kuungana nanyi mwaka mzima wa shule na ninawahimiza kusoma vifaa vyote vya HSD kwa umakini.

Asante kwa kujitolea kwako bila kusita kwa Wilaya ya Shule ya Hazelwood.

Kwa Dhati

Dr. Nettie Collins-Hart  
Mrakibu

15955 Newv Halls Ferry Road. Florissant MO 63031  
314-953-5000  
Relay 800-735-2466  
**[www.hazelwoodschools.org](http://www.hazelwoodschools.org)**

## **TAARIFA ZA DHAMIRA, MAONO NA THAMANI**

### **TAARIFA ZA DHAMIRA**

Katika utamaduni wa matarajio makubwa na ubora, wanafunzi wetu watakuwa wa wa wasomi wa maisha wenye ujuzi za Karne ya 21 kwa mafanikio kama raia wa kimataifa.

### **TAARIFA YA MAONO**

Wilaya ya Shule ya Hazelwood inaendeleza wafahamu wa utamaduni wa fikra muhimu walio tayari kuongoza na ujuzi za karne ya 21 katika jamii ya dunia inayobadilika daima.

### **TAARIFA YA THAMANI**

- \* Mafanikio ya juu ya wanafunzi kulingana na vipimo nyingi tunapo tayarisha wanafunzi kuwa raia wa kimataifa.
- \* Wafanyakazi mbalimbali ambao wanajali, wenye uwezo wa kitamaduni, wenye mafunzo mazuri, na walio na ufanisi mkubwa katika majukumu yao.
- \* Kujiwajibisha wenyewe kwa utamaduni wa ubora na viwango vya juu katika kitaaluma na tabia.
- \* Kudumisha jukumu la hazina ya mali na rasilimali za wilaya huku tukitumia njia bora za kifedha.
- \* Mazingira ya kusaidia kwa mafunzo ambayo yanakuza maendeleo ya afya nzuri ya kijamii-kihisia kwa wanafunzi wote.
- \* Kutayarisha wanafunzi wenye fikra na ujuzi wa kimataifa ili kuwafanya wawe na tija chuoni, kwa kazi, na maisha katika karne ya 21.
- \* Ushiriki wa jamii unaoendesha ushiriki mkubwa wa wazazi na jamii / wadau, ushirikiano mzuri, na mahusiano mazuri na mawasiliano ya habari nyingi.

# KIJITABU CHA MAELEZO

## MAHUDHURIO

Bodi ya Wilaya ya Shule ya Hazelwood inatambua umuhimu wa mahudhurio ya kawaida ya wanafunzi kwa uzoefu wa mafunzo ya mafanikio. Mikondo za mahudhurio za kawaida na kufika kwa saa yatarajiwa kwa kila mwanafunzi aliyeandikishwa katika Wilaya ya Shule ya Hazelwood. Mwanafunzi wako asipokuwepo, tafadhali hakikisha kuwa unawasiliana na shule ya mtoto wako.

## **KUTOKUWEPO**

Kutokuwepo kwa Kuruhusiwa Simu kutoka kwa mzazi au cheti itahitajika

- Mwanafunzi kuugua
- Kifo katika familia ya mwanafunzi au rafiki wa karibu
- Siku fulani kwa ajili ya kaidi ya kidini
- Miadi za daktari au meno
  - \* Ikiwa mwanafunzi anahitaji kupanga mapema kutokuwepo, (yaani, akienda safari, miadi ya daktari, na kadhalika), lazima awasilishe taarifa ya maandishi na saina ya mzazi wake siku moja kabla ya kutokuwepo, au kabla ya shule, ikiwa mwanafunzi anapanga kutoka shuleni mchana. Cheti hii lazima ieleze saa na tarehe ambayo mwanafunzi ataondoka na lazima ijumuishe namba ya simu ambapo wazazi wanaweza kufikiwa kwa uthibitisho. Inapendekezwa kwamba wazazi wafanye miadi ya meno na daktari baada ya masaa ya shule.
- Kwenda kotini
- Karantini au kuwekwa hospitalini
- Kutokuwepo na idhini ya awali, (yaani, kushiriki katika fursa halali ya elimu, kama vile ziara ya chuo kikuu)
- Safari ya masomo za nje au kutokuwepo kwa sababu zingine zilizoanzishwa na shule
- Dharura au seti ya hali ambazo, kwa uamuzi wa mkuu wa shule, inajumuisha sababu nzuri ya kutokuwepo shuleni, (kulala zaidi, shida ya gari, kuendesha shughuli za wazazi, uangalizi wa watoto kwa kawaida haichukuliwi kuwa ya dharura).
- Kazi ya utawala na mahudhurio katika programu ulioidhinishwa na Wilaya (yaani, Kituo cha Msaada Mbadala, Kusimamishwa Shule, Programu Chanya ya Kuchagua

Ikiwezekana, mwanafunzi ataruhusiwa kufanya kazi ya muda uliopotea iliyokosekana kutokana na kutokuwepo kwa kuruhusiwa, isipokuwa kama kazi ilikuwa shughuli ya darasa nzima (yaani, safari ya masomo ya nje, maabara, au mazoezi ya kimwili). Katika mazingira hayo, hakuna adhabu itakayowekwa kwenye alama ya mwanafunzi; badala yake, kazi mbadala katika kiwango hicho hicho cha ugumu inapaswa kutolewa na mwalimu.

Kutokuwepo Bila: Ruhusa Kutokuwepo bila kuorodheshwa chini ya Kutokuwepo kwa Kuruhusiwa inachukuliwa kuwa kutokuwepo bila ruhusa.

Kuondoka katika viwanja vya shule: Kwa ajili ya ulinzi wa mwanafunzi, mwanafunzi hataondoka katika viwanja vya shule kwa sababu yoyote ile, na mtu yeyote, bila ruhusa kutoka ofisini. Kabla ya mwanafunzi hajaondoka shuleni juu ya kutokuwepo iliyopangwa mapema au ugonjwa, mzazi

wa mwanafunzi, mlezi au mteuzi lazima aripoti ofisini na kusaini kumtoa mwanafunzi, au, kwa wanafunzi wanaoruhusiwa kuendesha gari shuleni, wazazi/walezi lazima watoe uthibitisho kwamba mwanafunzi anaruhusiwa kujisaini mwenyewe ili aondoke katika viwanja vya shule bila kuambatana. Wanafunzi wanaoondoka chuoni kwa wakati usiopangwa bila kufuata taratibu hizi watakabiliwa na hatua za kiadhibi kama ilivyoelezwa chini ya "Utoro".

Utoro: Wanafunzi wasiokuwa chuoni au darasani bila ufahumu au idhini ya wazazi/walezi na wasimamizi wa shule. Mzazi, mlezi au mlinzi wa mtoto au watoto ambao hawahudhuri shule kila mara wanaweza kuripotiwa kwenye Idara ya Watoto na/au Mfumo wa Mahakama ya Watoto. Ukiukaji wa sheria ya mahudhurio ya lazima ni kosa la daraja C: Utoro Sugu (rufaa kwa Mahakama ya Familia), na inafafanuliwa kama: mwanafunzi ambaye hayupo shuleni bila idhini kwa siku nzima au zaidi, sehemu ya siku, au yote au sehemu ya darasa zaidi ya mara 10 kwa mwaka wa shule.

## **TARATIBU ZA MAHUDHURIO**

### **SIMU YA KUTOKUWEPO**

Kuna laini ya simu ya asiyehudhuria inapatikana katika ofisi ya kila shule masaa 24 kwa siku. Unapaswa kupiga simu kwa nambari ya mahudhurio ya shule ya mtoto wako ili kuripoti kutokuwepo kwa mtoto wako. Tafadhali sema jina la mtoto, jina la mwalimu au nambari ya chumba na sababu ya kutokuwepo.

### **KURUHUSIWA KUONDOKA**

Hatupendekezi kuondoka mapema na kuomba kuwa miadi zote za matibabu zipangwe nje ya siku ya shule kila inapowezekana. Wanafunzi wanapaswa kuachiliwa kwenda tu na wazazi, walezi wa kisheria au wale walioidhinishwa nao hasa. Mtu mwingine mzimu yeyote anayeomba mwanafunzi aachiliwe ataombwa kitambulisho na mzazi kupigiwa simu. Wanafunzi wataruhusiwa kuondoka kutoka kwa ofisi za shule; SIO darasani. Wazazi lazima wa saini mtoto kutoka kwa ofisi.

**Wazazi wa Shule ya Msingi:** Ikiwa mtoto wako ataenda nyumbani kutoka shuleni kwa njia inayokiuka utaratibu wa kawaida, lazima uwasiliane na shule kwa maandishi siku hiyo. Ikiwa cheti haijapokelewa, mtoto wako atarudishwa nyumbani kwa njia ya kawaida.

**Wazazi wa Shule za Kati na Sekondari** Mwanafunzi hataachiliwa kwenda na ndugu, fafiki nk., bila cheti kutoka kwa mzazi kwa kila rufusa. Kila cheti itathibitishwa hivyo ni muhimu kuwa nambari ya mawasiliano ya simu ijumuishwe. Mtu yeyote anayemchukua mtoto wako lazima aonyeshe utambulisho unaofaa na kuorodheshwa kwenye taarifa ya mtu wa kuwasiliana wakati wa dharura kabla mtoto wako kuachiliwa.

## MASAA

|                  |                                |   |
|------------------|--------------------------------|---|
| Madarasa za K-5  | Shule Inaanza saa 2:50 asubuhi | Kuondoka saa 9:50 alasiri<br>Kuondoka Mapema saa 8:50 alasiri |
| Madarasa za 6-8  | Shule Inaanza saa 2:00 asubuhi | Kuondoka saa 9:00 alasiri<br>Kuondoka Mapema saa 8:00 alasiri |
| Madarasa za 9-12 | Shule Inaanza saa 1:15 asubuhi | Kuondoka saa 8:15 alasiri<br>Kuondoka Mapema saa 7:15 alasiri |

## KUWASILI KUCHELEWA

Wanafunzi wanaofika kuchelewa wanapaswa kuripoti kwa katibu wa mahudhurio katika ofisi kuu kupata karatasi ya kuchelewa ambayo itakabidhiwa kwa mwalimu wa darasa.

## KAZI YA MUDA ULIOPOTEA

Itakuwa ni jukumu la mwanafunzi na/au mzazi kuanzisha ombi la kazi ya muda uliopotea na kuanzisha nyakati kwa makubaliano na mwalimu kwa kazi ya kila siku na mtihani ya muda uliopotea.

## KUCHELEWA

Kuchelewa inafafanuliwa kama kuwasili shuleni, darasani au eneo lililopangiwa mwanafunzi kuchelewa. Mwanafunzi anapowasili shuleni baada ya kengele ya kuchelewa, lazima apitie ofisini kuchukua pasi kabla ya kwenda darasani.

## MAHITAJI YA MAHUDHURIO NA KURIPOTI

### MASUALA YA KISHERIA

Sheria ya Shule ya Missouri inaweka wazi mzigo wa jukumu la mahudhurio shuleni kwa mzazi au mlezi.

Sheria inawataka watoto wote wenye umri kati ya miaka 7 na 16 kila mara kuhudhuria shule ya umma, binafsi, parokia, shule ya nyumbani au mchanganyiko wa shule hizo kwa muda wa kipindi chote cha muhula wa shule. Wazazi wana jukumu la kuhitaji na kukuza mahudhurio ya shule ya mtoto wao kila, ambayo ni hatua ya kwanza katika kufikia mafanikio ya kitaaluma.

### MAWASILIANO

Taratibu za mahudhurio ya wilaya yatachapishwa kila mwaka na kupatikana na kila Familia ya Hazelwood Kwa ajili ulinzi wa mwanafunzi, mawasiliano yafuatayo yata yatatolewa:

### MAJUKUMU YA SHULE

- A. Kila shule itaweka kumbukumbu sahihi za mahudhurio ya kila siku ya mwanafunzi kama inavyotakiwa na Sheria ya Jimbo la Missouri. Taratibu za Mahudhurio ya Wanafunzi ya Wilaya zinapatikana katika kila jengo la shule.

- B. Kila shule itawajulisha wazazi/walezi juu ya wanafunzi kutokuwepo bila ruhusa na/au kutokuwepo kupita kiasi. Arifa ya mzazi inaweza kujumuisha, lakini haikomei kwa, mojawapo ya yafuatayo:
- Mifumo za Ujumbe wa Sauti
  - Mawasiliano na mwalimu
  - Wapiga simu wa Ofisi ya mahudhurio
  - Barua zinayozalishwa na kompyuta
  - Ripoti za maendeleo
  - Mawasiliano na msimamizi, mshauri au mfanyakazi wa kijamii
- C. Kila shule itatekeleza taratibu za mahudhurio ili kushughulikia kutokuwepo kupita kiasi na/au kutokuwepo bila ruhusa/kuchelewa. Hizi taratibu zinaweza kujumuisha yafuatayo:
- Arifa ya mwalimu kwa wazazi (yaani, notisi ya kukosa kuhudhuria, ripoti ya maendeleo, mawasiliano ya simu)
  - Mkutano wa wanafunzi-walimu
  - Mkutano wa wazazi
  - Wafanyakazi wa kusaidia (yaani, muuguzi wa shule, mshauri, mfanyakazi wa kijamii, msimamizi, timu ya utunzaji)
  - Rufaa ya Mahakama ya Watoto (kwa wale walio chini ya umri wa 16)

#### **MAJUKUMU YA MWALIMU**

- A. Kila mwalimu atawajibika kuchukua na kurekodi mahudhurio sahihi ya wanafunzi kila saa.
- B. Kila mwalimu atawajibika kufuatilia mahudhurio ya wanafunzi na kuwajulisha wazazi/walezi wakati ambapo alama za kozi ya mwanafunzi linaathiriwa vibaya na kutokuwepo kupita kiasi na/au kutokuwepo bila ruhusa/kuchelewa.
- C. Kila mwalimu atatekeleza taratibu na sera za mahudhurio ya Wilaya.
- D. Kila mwalimu atawaruhusu wanafunzi ruhusa ya kukosekana kubaki kwa darasa lao wakati huo ili kufanya kazi na, ikiwezekana, kuruhusu wanafunzi kufanya kazi ya muda uliopotea.

**KUMBUKA:** Mwanafunzi ambaye amesimamishwa kwa muda kupitia kwa programu ya Wilaya (yaani, Kituo cha Msaada Mbadala, Programu Chanya ya Kuchagua, Kusimamishwa kwa Muda Shuleni, Kizuizi cha Jumamosi, na/au Kusimamishwa kwa Muda na Mkuu wa Shule) atastahili kupata maksi za kitaaluma.

#### **MAJUKUMU MZAZI/MLEZI**

- A. Sheria ya Shule Missouri chini ya sehemu ya Mahudhurio ya Shule ya Lazima inaweka mzigo wa jukumu la mahudhurio ya shule kwa mzazi.
- "Kila mzazi, mlezi, au mtu mwingine katika jimbo hili aliye na mamlaka, udhibiti au ulinzi ya mtoto kati ya umri wa miaka 7 na 16 atamsababishia mtoto kuhudhuria kila mara baadhi shule ya umma, binafsi, parokia, au shule ya nyumbani kwa muda usiopungua muda wote muhula ya shule ambayo mtoto anahudhuria."  
(R.S.MO.167.031).
- B. Wazazi wataarifu ofisi ya mahudhurio ya shule kila wakati mwanafunzi asikuwepo. Simu inapaswa kupigwa kuthibitisha kutokuwepo siku hiyo.

- C. Wazazi/walezi watafanya mipango yanayohitajika ikiwa watapanga mapema ili kumtoa mwanafunzi shuleni.

**KUMBUKA:** Wazazi wanapaswa kuelewa kwamba haiwezekani kufanya mazoezi mengi za muda uliopotea zinazotokea wakati wa darasa (yaani, majadiliano, kazi ya maabara ya filamu, mazoezi ya muziki, mazoezi ya kimwili, na kadhalika).

### **MAJUKUMU YA MWANAFUNZI**

- A. Wanafunzi watafuata taratibu za mahudhurio kama ilivyofafanuliwa na kila shule.  
B. Wanafunzi watashirikiana na maafisa wa shule na wafanyakazi wa kusaidia kurekebisha matatizo yoyote ya mahudhurio ambayo yanaweza kutokezea.

**KUMBUKA:** Isipokuwa katika kesi ya kuwekwa chini ya utawala katika Programu ya Wilaya (yaani, Kituo cha Msaada Mbadala, Programu Choiceanya wa Kuchagua, na Kusimamishwa kwa Muda Wakati wa Shule), mwanafunzi au mzazi anawajibika kuanzisha ombi la kufanya kazi ya muda uliopotea kulingana na miongozo ya shule.

Wanafunzi wanapaswa kuelewa kwamba haiwezekani kufanya mazoezi mengi za muda uliopotea zinazotokea wakati wa darasa (yaani, majadiliano, kazi ya maabara ya filamu, mazoezi ya muziki, mazoezi ya kimwili, na kadhalika).

### **PROGRAMU ZA A+ ZA SHULE (SHULE ZA SEKONDARI)**

Shule zote za sekondari za Wilaya ya Shule ya Hazelwood zinachukuliwa kuwa shule za A+, ambazo zinaweza kuwapa wanafunzi motisha ya kifedha kuhudhuria vyuo vya jamii ya umma na shule za kiufundi. Wanafunzi lazima watimize miongozo ya A+ kama ilivyowekwa na jimbo la Missouri. Fedha zote zinategemea na serikali kutenga fedha.

#### **Miongozo ya sasa ni:**

- Kuwa raia wa Marekani, mkazi wa kudumu, au upo nchini Marekani kisheria.
- Ingia katika makubaliano ya maandishi na shule ya sekondari kabla ya kuhitimu
- Hudhuria shule iliyoteuliwa kwa miaka mitatu mfululizo kabla ya kuhitimu
- Kuhitimu na GPA ya jumla ya pointi 2.5 au zaidi kwa kipimo cha pointi 4
- Kuwa na jumla mahudhurio ya angalau asilimia 95 kwa Madarasa za 9-12
- Fanya masaa 50 ya mafunzo au ushauri isiyolipwa yanayosimamiwa na wilaya
- Weka kumbukumbu ya uraia mwema na kuepuka matumizi yasiyo halali ya dawa za kulevya na pombe
- Kupata alama ya ujuzi au ya juu zaidi kwenye mtihani wa Algebra I mwishoni mwa kozi

### **UTUNZAJI KABLA NA BAADA YA SHULE**

Shule zetu kadhaa zina utunzaji kabla na baada ya shule zinazotolewa na YMCA. Kwa taarifa za usajili, piga simu YMCA kupitia 521-1822.

## UONEVU/UNYANYASAJI

Ili kukuza mazingira salama ya masomo kwa wanafunzi wote, Wilaya ya Shule ya Hazelwood inapiga marafuku aina zote za uonevu/unyanyasaji. Wilaya pia inapiga marafuku kisasi au ulipizaji kisasi dhidi ya mtu yeyote anayeripoti kitendo cha uonevu/unyanyasaji miongoni mwa au dhidi ya wanafunzi.

### **Ufafanuzi**

**Uonevu/Unyanyasaji** - Kwa mujibu wa sheria za serikali, uonevu/unyanyasaji hufafanuliwa kama vitisho, tabia zisizohitajika za uchokozi, au unyanyasaji ambao ni wa kurudiwa au una uwezekano mkubwa wa kurudiwa na kusababisha mwanafunzi wa kawaida kuogopea usalama wake wa kimwili au vitu vyake; ambayo inaingilia kati ufaulu wa elimu, fursa au faida za mwanafunzi yeyote bila ubaguzi; au inavuruga kwa kiasi kikubwa uendeshaji wa shule kwa utaratibu unaofaa. uonevu/unyanyasaji unajumuisha, lakini haikomei kwa: vitendo vya kimwili, ikiwa ni pamoja na uhalifu, ishara, wizi, au uharibifu wa mali; mawasiliano ya kuongea, yaliyoandikwa, au ya elektroniki, ikiwa ni pamoja na kuchafua jina, matusi, unyama, au vitisho; au vitisho vya kisasi au kulipiza kisasi kwa ajili ya kuripoti matendo hayo.

**Uonevu/Unyanyasaji Mtandaoni** - Aina ya uonevu/unyanyasaji unaofanywa kwa kutuma mawasiliano ikiwa ni pamoja na, lakini haikomei kwa, ujumbe, maandishi, sauti au picha kwa njia ya kifaa cha elektroniki ikiwa ni pamoja na, lakini haikomei kwa, simu, simu ya upepo au vifaa vingine vya mawasiliano ya upepo, kompyuta au bipa. Wilaya ina mamlaka juu ya uonevu/unyanyasaji mtandaoni unaotumia rasilimali za teknolojia ya wilaya au inayoanza kwa ardhi na majengo ya wilaya, katika shughuli ya wilaya au kwenye usafiri wa wilaya. Hata wakati ambapo uonevu/unyanyasaji mtandaoni haihusishi ardhi na majengo ya wilaya, shughuli au rasilimali za teknolojia, wilaya itaweka matokeo na adhabu kwa wale wanajiingiza kwenye uonevu/unyanyasaji mtandaoni ikiwa kuna uhusiano wa kutosha kwa mazingira ya elimu, tabia inavuruga mazingira ya elimu kwa kiasi kikubwa, mawasiliano hayo yanahusisha tishio kama ilivyofafanuliwa na sheria, au wilaya inaruhusiwa vinginevyo na sheria kushughulikia tabia hiyo.

**Siku Shuleni** – Siku kwenye kalenda ya shule wakati wanafunzi wanatakiwa kuhudhuria shule.

### **Maafisa Walioteuliwa**

Mkuu wa kila jengo ameteuliwa kama mtu binafsi kupokea na kuchunguza ripoti za uonevu/unyanyasaji. Kila mkuu wa jengo atateua angalau walimu wawili au wasimamizi katika jengo ambao wamepeva mamlaka ya kupokea na kuchunguza ripoti za uonevu/unyanyasaji wakati ambapo mkuu hayupo au kwa hiari ya mkuu.

Afisa wa uzingatiaji wa wilaya aliyeteuliwa katika sera AC atahudumu kama mratibu wa kupambana na uonevu/unyanyasaji wilaya nzima. Mratibu huyo wa kupambana na uonevu/unyanyasaji atapokea ripoti za taarifa zote za uchunguzi zilizokamilika kutoka majengo yote na kuchambua ripoti ili kubaini taarifa zozote zitakazotoa taarifa zozote zitakazofahamisha kuelimisha juu ya kupambana na ubaguzi na kupambana na uonevu/unyanyasaji na programu za mafunzo. Kwa kuongezea, mratibu wa kupambana na uonevu/unyanyasaji atasaidia katika kutayarisha ripoti zozote husika kama inavyotakiwa na serikali na sheria za shirikisho.



## **Kuripoti Uonevu/Unyanyasaji**

Wafanyakazi wa shule, wabadala au wafanyakazi wa kujitolea wanatarajiwa kuingilia kati kuzuia uonevu/unyanyasaji wa wanafunzi, kuadhibu mhusika ipasavyo, kumsaidia mwathiriwa na kuripoti tukio hilo kwa mkuu wa jengo au mteuliwa kwa uchunguzi zaidi na hatua. Mfanyakazi yeyote wa shule, mbadala au wa kujitolea ambaye anashuhudia au ana habari ya moja kwa moja wa uonevu/unyanyasaji wa mwanafunzi lazima aripoti tukio hilo kwa mkuu wa jengo au mteuliwa haraka iwezekanavyo, lakani kabla siku mbili za shule hayajaisha baada ya tukio hilo.

Wanafunzi ambao wamefanyiwa uonevu/unyanyasaji, au ambao wameshuhudia au wana habari ya uonevu/unyanyasaji, wanahimizwa kuripoti mara moja matukio kama hayo kwa mfanyakazi wa shule. Mfanyakazi yeyote wa shule anayepokea ripoti hiyo ataipitisha mara moja kwa mkuu wa jengo au mteuliwa.

Ikiwa tukio la uonevu/unyanyasaji linahusisha wanafunzi kutoka zaidi ya jengo moja la wilaya, ripoti hiyo inapaswa kutumwa kwa mkuu au mteuliwa wa jengo ambalo tukio hilo lilitokea au, ikiwa inafaa zaidi, kwa mkuu au mteuliwa wa jengo lililohudhuriwa na washiriki wengi katika tukio hilo.

## **Uchunguzi**

Ndani ya siku mbili za shule baada ya kupokea ripoti ya uonevu/unyanyasaji, mkuu au mteuliwa ataanza uchunguzi wa tukio hilo. Ripoti zinazohusisha wanafunzi kutoka majengo mengi zitachunguzwa kwa ushirikiano na wakuu wa kila jengo linalohusika au wakuu hao wanaweza kuomba kwamba afisa wa uzingatiaji wa wilaya aliyeteuliwa katika sera AC kufanya uchunguzi. Ikiwa wakati wowote wa uchunguzi mkuu atapata kwamba uonevu/unyanyasaji unahusisha ubaguzi haramu, unyanyasaji au kulipiza kisasi kama ilivyoelezwa katika sera AC, mkuu huyo ataripoti tukio hilo kwa afisa wa uzingatiaji aliyeteuliwa katika sera hiyo, ambaye atasaidia katika uchunguzi. Ikiwa madai ya uonevu/unyanyasaji yanahusisha mwanafunzi maalum wa elimu au mwanafunzi mwenye ulemavu, mkuu pia atamwarifu mkurugenzi wa elimu maalum.

Uchunguzi huo utakamilika ndani ya siku kumi za shule baadaye ya tarehe ripoti ya uonevu/unyanyasaji kupokelewa isipokuwa kama sababu nzuri ipo ili kuongeza uchunguzi. Baada ya kukamilisha uchunguzi, mkuu ataamua kama uonevu/unyanyasaji au unyanyasaji ulitokea na, ikiwa ni hivyo, kama adhabu ya ziada inadhaminiwa kwa mujibu wa kanuni ya adhabu ya wanafunzi wa wilaya. Mkuu huyo atazalisha ripoti ya maandishi ya uchunguzi huo na yaliyopatikana na kutuma nakala ya ripoti iliyokamilika kwa mratibu wa kupambana na uonevu/unyanyasaji wilayani. Mkuu au mteuliwa ataandika ripoti katika mafaili ya mwathiriwa na madai au mhusika halisi wa uonevu/unyanyasaji. Ripoti zote zitawekwa siri kwa mujibu wa sheria za serikali na shirikisho.

Ikiwa tukio hilo lilihusisha madai ya ubaguzi haramu au unyanyasaji, uamuzi wa mkuu unaweza kupingwa kwa mujibu wa sera AC. Adhabu ya mwanafunzi inaweza kupingwa inaporuhusiwa na sheria kwa mujibu wa sera ya Bodi.

Mkuu au mtumishi mwingine wa wilaya anayefaa atashirikiana na waathirika na familia zao kufikia rasilimali na huduma ili kuwasaidia kukabiliana na athari zozote hasi zilizotokana na tukio hilo.

## **Matokeo**

Wanafunzi wanaoshiriki katika uonevu/unyanyasaji au wanaolipa kisasi dhidi ya yeyote atakayeripoti uonevu/unyanyasaji wataadhibiwa kwa mujibu wa kanuni za adhabu wilayani. Adhabu kama hiyo inaweza kujumuisha kuwekwa kizuizini, kusimamishwa kwa muda shuleni, kusimamishwa kwa muda nje ya shule, kufukuzwa, na kuondolewa kutoka ushiriki katika shughuli, kutengwa na heshima na tuzo, na matokeo mengine yanayoonekana kuwa sahihi na wakuu. Wilaya pia itawasiliana na watekezaji wa sheria inapotakiwa na sheria au kuarifu makampuni ya mitandao ya kijamii juu ya shughuli zisizofaa mtandaoni pale inapofaa.

Hata katika hali ambapo wilaya haina mamlaka ya kumwadhibu mwanafunzi kwa uonevu/unyanyasaji, kama pale ambapo matendo yanavyofanyika nje ya chuo na kuna uhusiano haitoshi kwa wilaya, mkuu au mteuliwa atachukua hatua zinazofaa kuwasaidia wanafunzi waathirika. Vitendo kama hivyo vinaweza kujumuisha, lakini haikomei kwa, kuwasiliana na wazazi/walezi wa mwathirika na wahusika wanaodaiwa, kuwasiliana kwamba tabia hii hairuhusiwi kwa viwanja vya wilaya au katika shughuli za wilaya, kuwajulisha watumishi sahihi wa wilaya kumsaidia mwathirika, na kuchukua hatua za ziada pale inapofaa, kama vile kuarifu watekelezaji wa sheria au kampuni za mitandao ya kijamii.

Wafanyakazi wa wilaya na wabadala wanaokiuka sera hii wataadhibiwa au kufutwa kazi. Adhabu inaweza kujumuisha kusimamishwa kwa muda na au bila malipo, tathmini hasi, na kupigwa marufuku kuwa kwa ardhi na majengo ya wilaya au katika shughuli za mafunzo zilizopewa na wilaya au hatua nyingine sahihi ya ziada. Wafanyakazi wa kujitolea wanaokiuka sera hii hawataruhusiwa tena kujitolea.

## **Chapisho la Sera**

Kila mwaka wilaya itawataarifu wanafunzi, wazazi/walezi, wafanyakazi wa wilaya, wabadala na wanaojitolea kuhusu sera hii na marufuku ya wilaya dhidi ya uonevu/unyanyasaji. Nakala ya sera hii itajumuishwa katika vitabu vya wanafunzi na kuwekwa kwenye tovuti ya wilaya.

## **Mafunzo na Elimu**

Mratibu wa kupambana na uonevu/unyanyasaji wilayani atatoa taarifa na mafunzo yanayofaa yaliyoundwa kusaidia wafanyakazi, wabadala, na wanaojitolea ambao wana mawasiliano makubwa na wanafunzi katika kutambua, kuzuia na kukabiliana na matukio za uonevu/unyanyasaji.

Wilaya itatoa elimu na taarifa za uonevu/unyanyasaji na sera hii kwa wanafunzi kila mwaka. Mkuu wa kila shule, kwa kushauriana na washauri wa shule na wafanyakazi wengine wa shule wanaofaa, wataamua mbinu bora za kuwezesha majadiliano. Mbinu zinaweza kujumuisha lakini haikomei kwa: mikusanyiko; maonyesho ya chumba cha darasa; mikutano ya darasa; mikutano ya timu au klabu; maonyesho maalum ya washauri, wafanyakazi wa kijamii au wataalamu wa afya ya akili; na matukio ya nyumba-wazi. Inapowezekana, wazazi/walezi wataalikwa kuhudhuria.

Kwa kuongezea kuwaelimisha wanafunzi kuhusu yaliyomo kwenye sera hii, wilaya itawajulisha wanafunzi juu ya:

- 1 Utaratibu wa kuripoti uonevu/unyanyasaji
- 2 Madhara ya uonevu/unyanyasaji.

- 3 Mirada zozote ambazo shule au wilaya imeunda kushughulikia uonevu/unyanyasaji, ikiwa ni pamoja na mipango ya rika kwa rika ya mwanafunzi.
- 4 Matokeo ya wale wanaoshiriki katika uonevu/unyanyasaji au kujihusisha na kisasi au kulipiza kisasi dhidi ya wale wanaoripoti uonevu/unyanyasaji.

Washauri wa shule, wafanyakazi wa kijamii, wataalamu wa afya ya akili, wanaoikolojia wa shule au watumishi wengine wa wilaya wanaofaa wataelimisha wanafunzi ambao ni waathirika wa uonevu/unyanyasaji kuhusu jinsi ya kushinda na athari hasi za uonevu ikiwa ni pamoja na, lakini haikomei kwa:

1. Kukuza thamani ya mwanafunzi na kujithamini.
2. Kumfundisha mwanafunzi kujihami kwa kulisimua na ufanisi na kwa ufanisi bila vurugu.
3. Kumsaidia mwanafunzi kukuza ujuzi wa kijamii
4. Kumtia moyo mwanafunzi kuendeleza nafasi ya ndani ya udhibiti.

#### Programu na Rasilimali za Ziada za Shule

Bodi inaelekeza mkuu au mteuliwa kutekeleza programu na miradi mingine ya kushughulikia uonevu/unyanyasaji, kujibu mwenendo kama huo kwa njia ambayo haimwaibishi mwathiriwa na kutoa rasilimali au rufaa zinazopatikana kwa waathirika wa uonevu/unyanyasaji. Miradi kama hiyo inaweza kujumuisha kuwaelimisha wazazi/walezi na familia juu ya kuzuia uonevu/unyanyasaji na rasilimali.

### **MKAHAWA NA HUDUMA ZA CHAKULA**

Huduma za mkahawa hutolewa wakati wa kifungua kinywa na chakula cha mchana. Kifungua kinywa na chakula cha mchana vyote vinapewa kukidhi mahitaji ya Idara ya Kilimo ya Marekani na ni pamoja na kinywaji cha kuchagua. Kifungua kinywa inatolewa bila malipo kwa wanafunzi wote wa shule ya msingi. Tafadhali nenda kwenye [www.hazelwoodschools.org](http://www.hazelwoodschools.org) kwa bei ya chakula cha mchana cha sasa. Shule zitaendelea na Mfumo wa Malipo ya Kabla ya Kompyuta kwa mlo kamili ya shule. Malipo yanaweza kufanywa kwa hundi au cheki. Tafadhali andika cheki zote kwa Wilaya ya Shule ya Hazelwood.

Wazazi wanaweza kuingia kwenye [www.myschoolbucks.com](http://www.myschoolbucks.com) na kulipa kabla chakula cha mtoto wao kwa kutumia kadi ya mkopo. Mara tu akaunti yako itakapoanzishwa, unaweza kuangalia salio na kuingiza pesa kwa akaunti kutoka kwa kompyuta, simu au faksi yako.

Wazazi wasio na intaneti wanaweza kupiga kupitia namba isiyo na tozo (1-855-832-5226) kupokea programu tumizi ya kulipa kwa simu au faksi.

Ndugu hawawezi kutumia akaunti ya mwingine bila ruhusa kutoka kwa Mkurugenzi wa Huduma za Chakula.

Wanafunzi wanaostahili faida ya chakula bila malipo hawatowi malipo yoyote. Wanafunzi wanaostahili chakula cha bei iliyopunguzwa lazima wafanye malipo ya kabla ya kiasi kilichorekebishwa kulingana na taratibu sawa na wanafunzi wengine wote. Wanafunzi lazima bado waingize nambari yao. Wanafunzi ambao hawana pesa katika akaunti yao watapatiwa sandwichi ya bure na chaguo ya kando na kinywaji.

Ili kupunguza kiasi cha matumizi ya karatasi na kuongeza ufanisi, Wilaya hainakili tena na kutuma menyu nyumbani. Menyu zinapatikana kwenye tovuti yetu katika [www.hazelwoodschools.org](http://www.hazelwoodschools.org). Wanafunzi wanaweza kuleta chakula chao cha mchana pia. Vyakula vya mchana vilivyoletwa kutoka nyumbani vinapaswa kufuata miongozo ya EatSmart ya Wilaya.

Taarifa kuhusu chakula cha bure/zilizopunguzwa zinapatikana katika ofisi ya shule.

## **SHULE YA MSINGI**

Tozo itafanywa dhidi ya akaunti hii kila wakati mwanafunzi anapoingiza namba yake kwenye kibao au kadi ya chakula cha mchana kutambazwa katika mashine ya malipo ya mkahawa. Wanafunzi wanapaswa kufundishwa ili kuweka nambari yao ya utambulisho siri. Wanafunzi wanakumbushwa wakati akaunti yao iko chini. Bahasha ya malipo ya kabla itatolewa kwa kila mtoto wakati akaunti inaonyesha kwamba mwanafunzi ana chakula cha mchana tatu tu iliobaki.

## **SHULE YA KATI / YA SEKONDARI**

Wilaya inatumia mfumo wa uhasibu wa chakula cha kompyuta. Mfumo huu unatambaza msimbo wa baa kwenye beji kitambulisho ya mwanafunzi; kwa hiyo, wanafunzi lazima waonyeshe na kutumia beji ya kitambulisho yao iliyetolewa na Wilaya kula kifungua kinywa na chakula cha mchana kila siku. Wanafunzi lazima walipe kabla kifungua kinywa/chakula cha mchana. Malipo ya kabla katika akaunti ya mwanafunzi yanaweza kufanywa kwa kupata bahasha ya malipo ya kabla kutoka kwa keshia wa mkahawa au kwa kuchukua moja toka ofisi za daraja la darasa. Wanafunzi ambao wako kwenye mpango wa chakula cha mchana wa bure au malipo yaliyopunguzwa lazima wawe na makaratasi ya kila mwaka yaliyojazwa na kurejeshwa kila mwaka. Kukosa kurudisha fomu hizi kwa wakati inaweza kusababisha kuchelewa kwa wanafunzi kupitishwa kwa chakula cha bure au bei zilizopunguzwa. Wanafunzi hawaruhusiwi kutoza chakula cha mchana. Wanafunzi wanaweza kuleta chakula chao cha mchana pia. Vyakula vya mchana vilivyoletwa kutoka nyumbani vinapaswa kufuata miongozo ya EatSmart ya Wilaya.

## **UNYANYASAJI NA KUTOTUNZA WATOTO**

Sheria ya Missouri inahitaji kwamba wasimamizi wa shule, washauri, au walimu watoe taarifa ya matukio yote anayoshukiwa ya unyanyasaji au kutotunza watoto kwa mamlaka ya kisheria yanayofaa. Mfanyakazi yeyote wa shule, anayefuatilia utendaji wa kazi zake, akiwa na sababu nzuri ya kuamini kwamba mtoto anayekuja mbele zake ana majeraha ya kimwili ambayo huenda yamesababishwa na mtu anayehusika na utunzaji wa mtoto, lazima aarifu Idara ya Watoto na mtawala anayesimamia mtoto.

## **URAIA NA ADHABU**

Wanafunzi na walimu wana majukumu tofauti katika mazingira ya shule. Wanafunzi wanahitaji kukumbuka majukumu haya na kuelewa kwamba Wakiwa shuleni, mwalimu anatumika kama mwenye mamlaka.

Sheria inawapa walimu mamlaka makubwa juu ya udhibiti na elimu ya mtoto, pindi mtoto amepolekwa shule na mzazi. Wanafunzi wanatarajiwa kuwa na heshima kwa wanafunzi wote, kitivo, na wafanyakazi: walimu, wakuu, washauri, wafanyakazi wa mkahawa, walinzi, maafisa wa usalama, nk, na wageni katika jengo hilo. Wanafunzi wanapaswa kufuata maelekezo ya kitivo na wafanyakazi baada ya ombi la kwanza kwa njia chanya (hakuna kurudisha maneno, ishara za

ujeuri, au uharibifu wa ardhi na majengo ya shule). Tabia na vitendo vya ujeuri, kukosa heshima, na lugha ya vurugu yenye uwezekano, havitavumiliwa na vitasababisha hatua ya adhabu inayofaa.

### **USHIRIKI WA RIADHA NA MWENENDO KATIKA TUKIO**

Kustahili kushiriki katika riadha na mazoezi za shule ni fursa—sio haki ya asili—inayotolewa ikiwa utakidhi viwango vya kustahiki kama ilivyowekwa na Chama cha Mazoezi za Shule ya Sekondari ya Jimbo la Missouri (MSHSAA). Viwango vya kustahiki vya MSHSAA vinaweza kupatikana kwa [www.mshsaa.org](http://www.mshsaa.org) au umwone mkurugenzi wa shughuli za shule yako.

Mwanafunzi ambaye tabia yake au mwenendo ni kama vile inaiga ukashifu juu yake anaweza kuondolewa kutoka kwa timu.

Wanafunzi wanatarajiwa kufuata Kijitabu cha Maelekezo/Mwongozo wa Tabia cha Mwanafunzi-Mzazi wakati wa hafla zote zilizofadhiliwa na shule. Wanafunzi wanahimizwa kuonyesha roho ya shule kupitia njia chanya, kama vile kuvaa rangi za shule, mavazi, na kushangilia timu yao.

Tafadhali kuwa na heshima kwa watazamaji wote na timu zinazopingana na mashabiki wao. Ukiukaji wowote wa sera za shule unaweza kusababisha hatua za adhabu.

### **MAWASILIANO NA KUTEMBELEA SHULE**

#### **BODI YA ELIMU**

Angalia [www.hazelwoodschools.org](http://www.hazelwoodschools.org) sehemu ya "kuhusu sisi" kwa habari juu ya mikutano ya Bodi ya Elimu.

#### **MABADILIKO YA ANWANI AU NAMBARI YA SIMU**

Kwa usalama na ustawi wa mtoto wako, tafadhali julisha shule mara moja ikiwa una mabadiliko ya anwani na/au nambari ya simu ya nyumbani au kazini. Ikiwa una mabadiliko ya anwani, nyaraka za mabadiliko hayo lazima ziwasilishwe katika ofisi ya shule. Namba za simu za mkononi zinaweza pia kutumwa katika ofisi ya shule.

#### **KUWASILIANA NA WALIMU**

Wazazi wanaopenda kuwasiliana na mwalimu wa mtoto wao wanaweza kuita ofisi ya shule au sanduku la barua ya sauti ya mwalimu. Kuachia mwalimu ujumbe, piga 953-5203 (Ujumbe ya Haraka). Ikiwa unajua nambari ya barua ya sauti, itakuelekeza uingie sasa. Ikiwa haujui nambari ya barua ya sauti,

bonyeza 11, sikiliza na kisha uingize jina la mwisho likifuatiwa na jina la kwanza la mwalimu.

**WALIMU HAWATAPOKEA SIMU WAKATI WA DARASA.**

Tafadhali weka miadi ya mikutano na walimu mapema. Pia unaweza kutuma barua pepe kwa mwalimu. Nenda kwenye [www.hazelwoodschools.org](http://www.hazelwoodschools.org) kupata orodha ya barua pepe.

#### **MAWASILIANO YA KITIVO / WAFANYAKAZI**

Kitivo na wafanyakazi wanaweza kuwasiliana kupitia barua sauti au barua pepe. Nambari za barua ya sauti na anwani za barua pepe zinaweza kupatikana kwenye ukurasa wa tovuti ya shule.

Unapotumia mfumo wa barua ya sauti, tafadhali piga 314-953-5203, na kisha ingiza tarakimu-tano za nambari ya barua ya sauti ya mwalimu. Ikiwa haujui nambari barua ya sauti ya mwalimu, unaweza kufikia orodha ya majina kwa kubonyeza "11" na kisha ingiza jina la mwisho la mwalimu. Kitivo na wafanyakazi watafanya kila juhudi kujibu barua ya sauti yako au barua pepe mara moja.

Fursa za kujumuika na mkuu, mwalimu au mshauri zinapatikana wakati wa mikutano wazi ya nyumba, mikutano za mzazi/mwalimu, au kwa kuweka miadi. Unaweza kumpigia simu mtu ambaye ungependa kukutana naye na kupanga wakati rahisi kwenu wote. Tafadhali fahamu kwamba utahitaji kusaini katika ofisi kuu ikiwa unakutana na mwanachama wa kitivo na kusubiri maelekezo.

**Wakuu Wasaidizi:** Katika shule zote za kati na za sekondari, na baadhi ya shule za msingi, wanafunzi hupewa mkuu msaidizi wanapojisajilisha. Jukumu la mkuu msaidizi katika shule ni kuwa kiongozi wa maelekezo. Walimu wanapofanya kazi na kila mwanafunzi kutatua masuala ya adhabu, mkuu msaidizi anaweza kuitwa kuingilia kati kwa hali fulani. Mkuu msaidizi atafuata Kijitabu cha Maelekezo/Mwongozo wa Tabia cha Mwanafunzi-Mzazi wakati wa kukabiliana na tabia mbaya na ukiukaji kwa wanafunzi.

**Washauri:** Wanafunzi wanapewa mshauri wa mwongozo wanapojisajilisha. Jukumu la mshauri shuleni ni kutoa msaada na mwongozo unaohitajika ili kusaidia kuwezesha mafanikio na kushughulikia masuala yoyote ya kitaaluma, kazi, elimu, wasiwasi ya kibinafsi/au ya kijamii. Washauri wamefunzwa kusimamia na kutafsiri vipimo vya majaribio ya nia ya kielimu na kazi na tafiti na kutoa ushauri wa kibinafsi, kikundi, na mgogoro. Unaweza kuwasiliana na mshauri wa mtoto wako ikiwa una wasiwasi au maswali, au kupiga simu na kuweka miadi.

## **MIKUTANO ZA WAZAZI**

Kadi za ripoti za robo-mwaka ya kwanza zinapeanwa wakati wa mikutano ya wazazi-walimu. Mikutano ya ziada yanapendekezwa wakati wowote mwalimu au mzazi anapohisi mawasiliano yanahitaji kuwezesha kupitia mawasiliano ya moja kwa moja.

## **KITUO CHA WAZAZI MTANDAONI**

Kituo cha wazazi ni tovuti inayotegemea wavuti, inayolindwa na nywila, ambayo haionyeshi tu kazi ya kufanyia nyumbani na taarifa za alama, unaweza pia kuona habari za chanjo, mahudhurio, na adhabu ya mwanafunzi wako. Angalia tovuti yetu katika [www.hazelwoodschools.org](http://www.hazelwoodschools.org) kwa taarifa ya ziada.

## **MATEMBEZI YA WAZAZI**

Wazazi wanahimizwa kutembelea shule; hata hivyo, ziara za madarasa binafsi lazima zipangwe mapema kwa kuwasiliana na mwalimu ili kupanga ziara. **KWA USALAMA WA WANAFUNZI WETU, WAGENI WOTE LAZIMA WAJIANDIKISHE KATIKA OFISI YA SHULE BAADA YA KUWASILI.** Tafadhali pitia ofisini baada ya ziara yako.

## **KADI ZA RIPOTI NA RIPOTI ZA MAENDELEO**

Kadi za ripoti hutolewa mara nne kwa mwaka. Ripoti za maendeleo ya katikati ya robo-mwaka zinatumiwa nyumbani na wanafunzi ambao wanadhibitisha matatizo ya kitaaluma au tabia. Ripoti za ziada za maendeleo zitatumiwa kama inavyohitajika.

Kadi za ripoti za shule za kati hutolewa mara tatu kwa mwaka. Ripoti za maendeleo ya katikati ya mihula mitatu zinatumiwa nyumbani na wanafunzi ambao wanadhibitisha matatizo ya kitaaluma au tabia. Ripoti za ziada za maendeleo zitatumiwa kama inavyohitajika.

## **SHULE KUFUNGWA KWA AJILI YA HEWA MBAYA—953-THELUJI**

Tafadhali tegea vituo vya redio na televisheni kama vile KMOX-1120 AM, KTVI-Channel 2, KMOV-Channel 4, KSDK-Channel 5, KPLR-Channel 11 na HSD-TV, kwa taarifa za shule kufutwa; au piga simu kwa **laini ya Theluji ya Shule ya Wilaya ya Hazelwood kupitia 953-SNOW. Pia unaweza kwenda kwenye tovuti ya Wilaya ya Shule ya Hazelwood, ukurasa wa Facebook, na akaunti za Twita kwa habari ya dakika-hadi-dakika ya shule kufungwa.** Aidha, pia utapokea simu inayo pigwa kiotomatiki kutoka kwa Wilaya. Isipokuwa kama ni lazima kabisa, tafadhali usiite shule kujua kama shule liko katika kikao. Simu kama hizo zinafunga laini za simu.

Ikiwa shule imefungwa au kuna kuachiliwa mapema kutokana na hali mbaya ya hewa au dharura, hakutakuwa na Y-Care. Hata hivyo, ikiwa kuachiliwa mapema ni kabla ya kutoka saa 8:50 p.m.-9:50 alasiri, au ikiwa mazoezi za baada ya shule na za jioni zitutuliwa mbali, **Y-Care itakuwa wazi**, na YMCA itawapigia simu wazazi na kuwauliza wachukue watoto wao. Hii pia imeelezwa katika kijitabu cha mzazi cha Y-Care.

## **MAWASILIANO YA SHULE-NA-NYUMBANI**

Mara kwa mara shule itatuma mawasiliano yaliyo na matangazo na taarifa maalum kuhusu shughuli za shule kupitia Peachjar, barua pepe, na simu za kiotomatiki. Ingia kwenye tovuti ya Hazelwood kwa taarifa kila-dakika kuhusu Wilaya. Kila shule ina ukurasa wa nyumbani kwenye tovuti. Tegea shughuli za shule na Wilaya kwenye HSD-TV. Jisajili kwa jarida la barua pepe la Wilaya, "HSD E-Mail Extra," [www.hazelwoodschoools.org](http://www.hazelwoodschoools.org)

Tafadhali angalia mara kwa mara kwa matangazo ya shule na kazi za darasa ambazo hutumwa nyumbani.

## **SIMU NA UJUMBE**

Simu za ofisi na madarasa ni za matumizi ya kibiashara lakini zinaweza kutumika ruhusa inapotolewa na mfanyakazi wa ofisi na/au mwalimu. Wanafunzi hawapaswi kutumia simu hizi bila ruhusa. Wazazi wanaombwa kutopiga simu na kuachia ujumbe wanafunzi isipokuwa katika wakati wa dharura.

## **MAHITAJI YA HUDUMA YA JAMII (SHULE ZA SEKONDARI)**

Wilaya ya Shule ya Hazelwood inajitahidi kuunda wanafunzi wanaojali na kujitolea ambao wataleta mabadiliko katika jamii nzima na watakuwa na sauti katika mabadiliko ya kijamii. Kwa hiyo, **wanafunzi wote wanaohudhuria miaka minne ya shule ya sekondari wanatakiwa kukamilisha masaa 50\*** ya huduma za jamii kabla ya kuhitimu na kuruhusiwa kushiriki katika sherehe za kuhitimu. Masaa haya yanaweza kukamilishwa katika mwaka wa shule au wakati wa mapumziko. Shughuli zote za huduma ya kijamii lazima ziidhinishwe mapema na mratibu wa huduma ya kijamii katika jengo lako. \*Kuhamisha masaa za wanafunzi yatagawiwa, kutegemea na muhula zilizokamilishwa katika shule ya sekondari ya Hazelwood.

## **MTAALA, KUWEKA ALAMA, NA KAZI YA KUFANYIA NYUMBANI**

Mtaala wa Wilaya ya Shule ya Hazelwood imetengenezwa kwa umakini na inaendelea kufanyiwa marekebisho ili kutoa programu kamili ambayo itawatayarisha vyema wanafunzi wetu kwa

ulimwengu wa kesho. Masomo ya msingi ni pamoja na sanaa ya lugha ya Kiingereza, hisabati, sayansi, na masomo ya kijamii. Wanafunzi pia hupokea mafunzo katika sanaa, muziki, afya, elimu ya kimwili, ujuzi wa kusoma, ujuzi wa maktaba, matumizi ya kompyuta, na shughuli za ushauri wa kikundi kupitia mtaala wa Mwongozo wa Mtindo ya Missouri.

Wilaya inaendana na mitaala, mafunzo, na tathmini ya Viwango vya Kujifunza Missouri. Taarifa zaidi mahususi kuhusu mtaala wa Wilaya zinaweza kufikiwa katika [www.hazelwoodschoools.org](http://www.hazelwoodschoools.org)

## **VIWANGO VYA KITAALUMA NA MIZANI YA KUWEKA ALAMA**

Viwango vya kitaaluma na sera za kuweka alama zimewekwa na Bodi ya Elimu ya Hazelwood ili kudumisha ubora wa hali ya juu ambao shule zetu zinajulikana. Wanafunzi wanatarajiwa kufanya kulingana na uwezo wao wa hali ya juu na wanafunzi wote wanatakiwa kuonyesha umahiri thabiti kwa kila ngazi ya darasa ili kupandishwa cheo. Kadi za ripoti hutumwa nyumbani mwishoni mwa kila kipindi cha kupewa alama ili kuwajulisha wazazi juu ya maendeleo ya kitaaluma ya mtoto wao, juhudi, mwenendo, na tabia za kazi. Alama katika viwango vya madarasa ya tatu hadi tano hupangiwa kulingana na makundi yafuatayo kwenye ukurasa ufuatao.

### **SHULE YA MSINGI**

#### **MIZANI YA KUWEKA ALAMA**

|   |               |
|---|---------------|
| A | 100 - 90      |
| B | 89 - 80       |
| C | 79 - 70       |
| D | 69 - 60       |
| F | 59 - Na Chini |

#### **TARATIBU ZA KUWEKA ALAMA**

Aina za alama zitakazotambuliwa na kurekodiwa kwa lengo la kubaini alama za robo mwaka na / au za mwisho ni pamoja na yafuatayo:

- 1 Majaribio ya kawaida au yaliyoandikwa, kama vile majaribio ya kitengo au tathmini zingine
- 2 Shughuli za mazoezi ya kibinafsi zinazokamilika shuleni
- 3 Miradi ya muda mrefu au kazi maalum ambayo inahitaji muda mkubwa wa wanafunzi, juhudi na utafiti.
- 4 Michango yanayotolewa na mwanafunzi anayeleleza uelewaji wa dhana au ujuzi maalum (mwanafunzi anaweza kuonyesha hii kwa maneno, kwa maandishi au kupitia thibitisho).

### **SHULE YA KATI**

#### **MIZANI YA KUWEKA ALAMA**

|   |               |
|---|---------------|
| A | 100 - 90      |
| B | 89 - 80       |
| C | 79 - 70       |
| D | 69 - 60       |
| F | 59 - Na Chini |



## **TARATIBU ZA KUWEKA ALAMA**

**Umbizo (30% ya alama) na Muhtasari (70% ya alama)**

### **Ufafanuzi wa Umbizo**

Tathmini zinazotumiwa kutoa mwelekeo wa uboreshaji na / au marekebisho ya programu ya mwanafunzi binafsi au darasa nzima. Walimu hutumia hizi "tathmini za kujifunza" ili kushauri na kuongoza mafunzo yao na kuwasaidia wanafunzi binafsi kuelewa vyema maeneo yake ya ujuzi au upungufu.

### **Ufafanuzi wa Muhtasari**

Tathmini zinazotumika kutoa taarifa kuhusu mafanikio ya mwanafunzi mwishoni mwa somo, kitengo au kipindi cha mafunzo.

Walimu hutumia hizi "tathmini za kujifunza" kuamua ufanisi wa njia yao ya kufundisha na kuboresha mafunzo ya wanafunzi. Tathmini huwasaidia wanafunzi kupata uelewaji wa kina wa kile walichojifunza na jinsi walivyojifunza vyema.

## **SHULE YA SEKONDARI**

### **MIZANI YA KUWEKA ALAMA**

|   |               |
|---|---------------|
| A | 100 - 90      |
| B | 89 - 80       |
| C | 79 - 70       |
| D | 69 - 60       |
| F | 59 - Na Chini |

**Mitiani za Mwisho Wa Kozi yatakua 15% ya alama ya mwanafunzi.**

## **TARATIBU ZA KUWEKA ALAMA – TATHMINI (MITIHANI)**

**Umbizo (30% ya alama) na Muhtasari (70% ya alama)**

### **Ufafanuzi wa Umbizo**

Tathmini za ubaini zilizoundwa kutoa mwelekeo wa uboreshaji na / au marekebisho kwa programu ya mwanafunzi binafsi au darasa nzima.

Matumizi ya vitendo - Walimu hutumia hizi "tathmini za kujifunza" kushauri na kuongoza mafunzo yao na kuwasaidia wanafunzi binafsi kuelewa zaidi maeneo yake ya ujuzi au upungufu.

### **Ufafanuzi wa Muhtasari**

Tathmini zilizoundwa kutoa taarifa kuhusu mafanikio ya mwanafunzi mwishoni mwa kipindi cha mafunzo.

Matumizi ya vitendo - Walimu hutumia hizi "tathmini za kujifunza" kuamua ufanisi wa njia yao ya kufundisha na kuboresha mafunzo ya wanafunzi. Tathmini huwasaidia wanafunzi kupata uelewaji wa kina wa kile walichojifunza na jinsi walivyojifunza vyema.

**Mpango wa Tathmini ya Wilaya (Sera IL)** unahitaji wanafunzi wote walioandikishwa katika Wilaya ya Shule ya Hazelwood kushiriki katika tathmini zote za jimbo nzima.

*Tafadhali rejea kwa Sera IL, inapatikana kwenye tovuti ya Wilaya.*

| <b>Rasimu Mbaya</b>                    | <b>Mifano ya Muhtasari</b>         |
|--|------------------------------------|
| • Kazi ya kufanyia nyumbani*           | • Kazi ya kufanyia nyumbani*       |
| • Chemshabongo*                        | • Chemshabongo*                    |
| • Miradi*                              | • Miradi*                          |
| • Mawasilisho*                         | • Mawasilisho*                     |
| • Kuiga Mwingine (Mazoezi)*            | • Kuiga Mwingine*                  |
| • Maabara*                             | • Maabara*                         |
| • Maonyesho*                           | • Maonyesho*                       |
| • Insha*                               | • Insha*                           |
| • Hotuba*                              | • Hotuba*                          |
| • Tathmini ya Rika*                    | • Tathmini ya Rika*                |
| • Miradi za Kikundi                    | • Majaribio                        |
| • Tathmini za Umbizo za Kawaida        | • Mjadala                          |
| • Shughuli za Darasani                 | • Miradi za Utafiti                |
| • Changamsho (Kukamilisha / Kushiriki) | • Miradi za Kibinafsi              |
| • Daftari/Shajara (Kukamilisha &       | • Mitihani za EOC                  |
| • Ubora)                               | • Ripoti za Vitabu                 |
| • Ushiriki                             | • Jitihada za Tovuti               |
| • Majadiliano                          | • Mkusanyiko                       |
| • Kazi ya kengele                      | • Tathmini za Muhtasari za Kawaida |
| • Kazi Darasani                        |                                    |
| • Rasimu Mbaya                         |                                    |
| • Semina ya Socrate                    |                                    |
| • Maigizo (Muziki, Sanaa / Kucheza)    |                                    |
| • Kuongezewa/Alama ya Ziada            |                                    |
| • Kazi ya Kikundi                      |                                    |

\*Inamaanisha vipengele ambavyo vilipendekezwa kwa Tathmini ya Umbizo na Muhtasari.

#### **TARATIBU ZA KUWEKA ALAMA ZA MARUDIO “BADO”**

- Wanafunzi wote watapewa fursa ya jaribio moja kwa kila tathmini ya kurudia tathmini ili kuboresha asilimia yao. Hii haihusu katikati ya muhula, fainali na majaribio yanayowekwa alama nje ya Wilaya.
- Mwanafunzi yeyote anayeomba kurudia tathmini lazima apange na mwalimu na kuhudhuria (ma)kikao cha usaidzi kabla, wakati wa, au baada ya shule kwa shule ya kati/sekondari au kupata msaada wa ziada kutoka kwa mwalimu katika shule ya msingi. (Hii itahakikisha kuwa msaada unaohitajika unatolewa kabla ya kuchukua utathmini).
- Utathmini wote lazima ukamilike kabla ya tathmini inayofuata. \*Mpango wa Elimu ya Mtu Binafsi (IEP) au mpango wa 504 unaweza kutangulia mwongozo huu.
- Alama ya mwisho ya mwanafunzi kwa tathmini hiyo itakuwa ya juu kati ya alama hizo mbili.

## **KAZI YA KUFANYIA NYUMBANI\***

Kazi ya kufanyia nyumbani ni sehemu shule inayohitajika. Wanafunzi watatarajiwa kutumia muda kufanya kazi ya kufanyia nyumbani pamoja na kuhudhuria madarasa yao yaliyopangwa ili kufikia maendeleo ya kuridhisha. Baadhi ya kazi ni za muda mrefu katika asili na zinahitaji muda uliopangwa wa kusoma ili kukamilika. Wanafunzi wanahimizwa sana kukuza tabia nzuri za kusoma. Marafiki wa kusoma pamoja katika kila darasa ni muhimu ili kujadili au kupata kazi uliokasa wakati haupo. Sera za kazi ya kufanyia nyumbani zinatengenezwa katika kila darasa au timu ya kiwango cha darasa ili kukuza mafanikio na mafunzo ya wanafunzi wote na kuzuia alama kushindwa. Wazazi wanakumbushwa kwamba kusoma kila siku ni sehemu ya kazi ya kufanyia nyumbani.

## **MANTIKI YA TARATIBU ZA KAZI ZA NYUMBANI**

Kazi ya kufanyia nyumbani inatoa yafuatayo:

- Fursa ya masomo huru.
- Fursa kwa wanafunzi kuendeleza tabia za masomo ambazo zitawahudumia kwa maisha yao yote.
- Mawazo kwamba kujifunza haiaanzi au kuishia shuleni, lakini ni mchakato wa kuendelea maisha.

## **MADHUMUNI YA KAZI YA KUFANYIA NYUMBANI**

- Mazoezi - kuwasaidia wanafunzi kumudu ujuzi maalum ambazo zimewasilishwa darasani;
- Mwendo na usahihi wa wanafunzi unaongezeka na mazoezi.
- Matayarisho – kuwasaidia wanafunzi kupata faida za juu kutoka kwa masomo ya baadaye na / au kuweka malengo ya kujifunza.
- Nyongeza - kuwapa wanafunzi fursa ya kuhamisha ujuzi maalum au dhana kwa hali mpya kupitia utafiti, kulinganisha vipengele, kujenga msaada kwa hoja na kuwakilisha maarifa katika waandaaji wa mchoro
- Ubunifu/Matumizi - kuhitaji wanafunzi kuunganisha ujuzi na dhana nyingi ili kuzalisha majibu ya mwanzo.

## **MIONGOZO YA JUMLA YA KAZI YA KUFANYIA NYUMBANI**

- Wanafunzi wote wanatarajiwa kukamilisha kazi ya kufanyia nyumbani zilizopangiwa kwa ubora wa uwezo wao na kwa wakati.
- Kila zoezi la kazi ya kufanyia nyumbani litatathminiwa na kurudishwa kwa wanafunzi kwa wakati unaofaa.
- kazi ya kufanyia nyumbani zinapaswa kuhusiana moja kwa moja na mafunzo darasani na kufaa kwa mwanafunzi binafsi. Kwa hivyo, kazi za nyumbani zinapaswa:
  - kutopangiwa kama kipimo cha adhabu (Sera ya Wilaya)
  - kutambua kuwa muda wa mwanafunzi kusoma nyumbani naweza kuhitaji kugawanywa miongoni mwa masomo kadhaa na haipaswi kupita kiasi
- Wakati wa kupanga kazi za muda mrefu waalimu wanapaswa:
  - weka ratiba ya muda wa kazi na vituo vya ukaguzi ambavyo yatamsaidia mwalimu, mzazi na mwanafunzi kufuatilia maendeleo
  - kutoa maoni ya kutosha na kwa wakati kwa wanafunzi ili iwaruhusu kufanya masahihisho ya kazi katikati

- Wastani (jumla kila usiku) wa urefu wa muda inayopendekezwa kwa kila kiwango cha darasa ni:

|                  |                    |
|------------------|--------------------|
| La 1 = dakika 10 | La 7 = dakika 70   |
| La 2 = dakika 20 | La 8 = dakika 80   |
| La 3 = dakika 30 | La 9 = dakika 90   |
| La 4 = dakika 40 | La 10 = dakika 100 |
| La 5 = dakika 50 | La 11 = dakika 110 |
| La 6 = dakika 60 | La 12 = dakika 120 |

\* Ni vigumu kusimamia kikamilifu kazi ya kufanyia nyumbani, kwa muda au kiasi.

### MAJUKUMU YA MWALIMU

- Kutoa majukumu yenye maana ambayo yanaimarisha dhana, kuhamamisha ubunifu, na kukuza ujuzi muhimu za fikra au kuwapa wanafunzi fursa ya kupanua ujuzi wao wa somo. Kazi hizi zinapaswa kuongezeka kwa ugumu kiwango cha darasa na ujuzi cha mwanafunzi vinapoongezeka.
- Kutathmini mazoea ya kazi ya kufanyia nyumbani mara kwa mara. Hii inapaswa kufanyika kama matokeo ya asili ya mchakato wa kutathmini, kutathmini, na kupanga somo.
- Fanya kila juhudi kuhakikisha kwamba kazi za kufanyia nyumbani zinafafanuliwa na kueleweka wazi na wanafunzi wakati wa kupewa.
- Kubaliana na wazazi kuhusu wasiwasi za kazi za kufanyia nyumbani zinapojitokeza.
- Kuwa na kazi sahihi zipatikane ili kukamilishwa na wanafunzi ambao hawakuwepo.
- Dumisha kumbukumbu sahihi kwa wazazi kufikia kupitia Kituo cha Mzazi mtandaoni.
- Toa alama kwa kazi ya kufanyia nyumbani inayofaa kazi iliyofanywa na kuwapa wanafunzi fursa ya kurudia (onyesha ujuzi) kazi waliyopangiwa.
- Kufanya kazi kama wafanyakazi kutengeneza ili taratibu ili kuhakikisha kuwa kazi za kufanyia nyumbani zinaratibiwa kati ya masomo mbalimbali.

### MAJUKUMU YA MZAZI

- Onyesha hamu katika maendeleo na shughuli za mtoto wako shuleni.
- Wasiliana na mwalimu, mshauri, au msimamizi ikiwa matatizo yanatokea kuhusu kazi za kufanyia nyumbani.
- Toa sehemu inayofaa, yenye mwangaza mzuri, na utulivu na vifaa mwafaka kwa mtoto wako kusoma.
- Msaidie mwanafunzi kusimamia muda wa kazi za kufanyia nyumbani, pamoja na kazi za kila siku, mapendeleo, shughuli za shule, ajira, na burudani.
- Mhimize mtoto wako kuuliza maswali na kuomba msaada wa mwalimu kama haelewi wazi kazi au somo.
- Toa mwongozo na mapendekezo, lakini epuka majaribu ya kufanya tatizo, kuandika insha, au kufanya utafiti ya mwanafunzi.
- Kukubali tabia na juhudi za kazi za kufanyia nyumbani kwa sifa.
- Wasiliana na shule na/au walimu kwa kazi za marudio zinapofaa.

## **MAJUKUMU YA MWANAFUNZI**

- Wanafunzi wote wa shule ya sekondari wanatarajiwa kukamilisha kazi ya kufanyia nyumbani alizopangiwa kwa ubora wa uwezo wao na kwa wakati.
- Elewa kazi ya kufanyia nyumbani kabla ya kuondoka shuleni.
- Chukua nyumbani vifaa vyote vinavyohitajika ili kukamilisha (ma)zoezi hilo(zo).
- Ratibu muda bila vurugu na sambamba na shughuli za familia na/au za baada ya shule.
- Kamilisha kazi ya kufanyia nyumbani kwa wakati na kwa uwezo wako bora kila kila wakati.
- Ongea na (m)walimu kuhusu wasiwasi juu ya kazi ya kufanyia nyumbani.
- Wasiliana na shule na/au walimu kwa kazi za marudio zinapofaa.
- Simamia muda wa kazi ya kufanyia nyumbani, pamoja na kazi za kila siku, mapendeleo, shughuli za shule, ajira, na burudani.
- Wajibika kupata kazi ya kufanyia nyumbani zinazokosekana kutoka kwa mwalimu.

## **MIONGOZO YA KAZI YA KUFANYIA NYUMBANI KUCHELEWA**

- Wanafunzi ambao wamekosa kazi kutokana na “kutokuwepo kwa kuruhusiwa” watapewa idadi sawa ya siku za kurudisha kazi zilizokamilishwa kadri ya siku za kutokuwepo. Kwa mfano, ikiwa mwanafunzi hayupo siku 5 za shule, basi atakuwa na siku 5 za shule ya kurudisha kazi hizo. Muda wa ziada unaweza kutolewa kwa hiari ya mwalimu.
- Ni wajibu wa mwanafunzi kupata kazi za kufanyia nyumbani zinazokosekana kutoka kwa mwalimu.

## **KANUNI YA MAVAZI**

Wanafunzi lazima waje shuleni wakiwa wamevalia mavazi sahihi kila siku. Mapambo ya wanafunzi yanatarajiwa kuwa maridadi, safi na za kuvutia ili kila mwanafunzi aweze kushiriki katika kukuza mazingira mazuri, yenye afya na salama.

Wanafunzi wanapaswa kuitikia ipasavyo ombi lolote la busara linalohusisha na msimbo wa mavazi kutoka kwa wafanyakazi. Wakati, kwa maoni ya mkuu, mwanafunzi anavyoonekana au hali ya mavazi yanayovuruga mchakato wa elimu, au kuleta tishio kwa afya au usalama, mwanafunzi anaweza kuhitajika kufanya mabadiliko. Tafadhali rudi kwa Kijitabu cha Maelekezo/Mwongozo wa Tabia cha Mwanafunzi-Mzazi kwa maelezo zaidi juu ya msimbo wa mavazi na hatua za adhabu. Kuwa shuleni kwa sare, wanafunzi wanatarajiwa kuzingatia sera ya sare za shule.

## **SARE ZA SHULE**

Shule zifuatazo zimepitisha sera ya sare za shule nzima:

Shule za Msingi: Arrowpoint, Barrington, Brown, Grannemann, Garrett, Jamestown, Keeven, Larimore, Lusher, Townsend, na Twillman

Shule za Kati: Central Middle, North Middle, na Southeast Middle

## **KUFUNGWA KWA DHARURA NA KURUHUSIWA KUONDOKA MAPEMA**

### **KURUHUSIWA KUONDOKA MAPEMA KUTOKANA NA DHARURA**

Mara kwa mara, kuondoka mapema kwa wanafunzi kutatokea. Hakikisha kuwa na mipango uliyofanywa ya utunzaji wa mtoto wako shule ikipaswa kuruhusu kuondoka mapema kuliko kawaida. Hii ni pamoja na usafiri salama kutoka shuleni kwa wanafunzi ambao hawasafiri kwa basi. Kuondoka mapema hufuta shughuli zote za usiku, ikiwa ni pamoja na mazoezi.

Ikiwa shule imefungwa au kuna kuachiliwa mapema kutokana na hali mbaya ya hewa au dharura, hakutakuwa na Y-Care. Hata hivyo, ikiwa kuachiliwa mapema ni kabla ya saa ya kutoka 8:50 - 9:50 alasiri, au ikiwa mazoezi za baada ya shule na za jioni zimefutwa, **Y-Care itakuwa wazi**, na YMCA itawaita wazazi na kuwauliza wachukue watoto wao. Hii pia imeelezwa katika kijitabu cha mzazi cha Y-Care.

### **MAWASILIANO YA DHARURA**

Ikiwa shule inafungwa mapema kutokana na hali mbaya ya hewa au majanga mengine ya asili, au ikiwa dharura inahusiana na mtoto wako, tafadhali hakikisha umeorodhesha majina matatu na nambari za simu za ziada ya mawasiliano ya dharura. Arifu ofisi ya shule ikiwa nambari yoyote imebadilika.

### **MAZOEZI ZA WAKATI WA DHARURA**

Kila shule katika Wilaya ya Shule ya Hazelwood lazima ifanye mazoezi za wakati wa dharura kwa hali mbaya ya hewa, tetemeko la ardhi, vitisho vya bomu na wavamiaji. Kila shule ina mpango wa dharura wa kibinafsi.

### **SAFARI ZA MASOMO YA NJE**

Wanafunzi wanaweza kupewa fursa ya kushiriki katika safari za masomo ya nje mwaka mzima. Ni wajibu wa mwanafunzi kurudisha karatasi ya ruhusa iliyoandikwa na ada kwa tarehe iliyowekwa. Kukosa kurudisha makaratasi na ada zinazohitajika inaweza kusababisha mwanafunzi kutoshiriki katika shughuli hiyo. Waalimu wanaweza kuweka vigezo vya ustahiki wa mwanafunzi kwa safari ya masomo ya nje. Vigezo hivi vinaweza kujumuisha lakini haikomei kwa, mahudhurio, utendaji wa kitaaluma, na tabia. Mahudhurio shuleni siku ya safari ya masomo ya nje yanatarajiwa hata kama mwanafunzi atachagua kutoshiriki au haruhusiwi kushiriki katika safari ya masomo ya nje. Shughuli za maana zitatolewa. Wanafunzi wanawajibika kwa kazi zote zilizokosekana kutokana na kushiriki katika safari ya masomo ya nje.

### **MWELEKEO NA HUDUMA ZA USHAURI**

Mwelekeo na huduma za ushauri kama vile msaada wa kupanga elimu, utafsiri wa alama za mtihani, habari za ajira, msaada wa kitaaluma, na msaada wa wasiwasi nyumbani na/au kijamii zinapatikana kwa wanafunzi wote katika Wilaya ya Shule ya Hazelwood. Washauri pia wanaweza kufikia habari juu ya huduma za jamii zinazotoa msaada na kufanya vikundi vya usaidizi kwa msingi wa anayehitaji. Washauri watasaidia kupatanisha migogoro ya wanafunzi na kufanya kazi

na wanafunzi katika mazingira ya darasa ili kutoa taarifa juu ya masuala ambayo wanafunzi wanakabiliana nayo kila siku. Wanafunzi ambao wangependa huduma za mwongozo wanaweza kufanya miadi ya kutembelea mshauri wao kwa kufuata utaratibu wa shule zao au wazazi wao kupigia simu shule. Shule za Wilaya ya Hazelwood pia zina mtumishi wa kijamii anayepatikana ambaye anashirikiana na wafanyakazi wa shule kusaidia katika masuala mbalimbali ya wanafunzi na familia.

### **PASI ZA UKUMBINI**

Wanafunzi hawaruhusiwi katika kumbi wakati wa darasa isipokuwa wakiambatana na mwalimu au akiwa na pasi ya ukumbini kutoka kwa mwalimu au mfanyakazi. Wanafunzi lazima wawe na pasi ili kuona mwalimu, mshauri, mkuu, au kutumia simu.

### **UNYANYASAJI**

Wanafunzi wote wanatarajiwa kutendana mema kwa upole, hadhi, na heshima. Hakuna wanafunzi wanayepaswa kufanyiwa unyanyasaji wa aina yoyote. Mwanafunzi yeyote anayeamini kuwa anahitaji msaada katika kusimamisha aina yoyote ya unyanyasaji ataripoti kwa maneno tukio hilo kwa mfanyakazi yeyote ambaye anajisikia sawa kujadili tukio hilo, au anaweza kuandika na kuwasilisha malalamiko kwa Fomu ya Maelezo ya Mwanafunzi. Iwapo uchunguzi wa kina utabaini kuwa unyanyasaji umetokea, matokeo ya haraka yatapimwa ambayo yanatoshana na ukali wa tukio hilo.

Matukio ya unyanyasaji yanayorudiwa yatasababisha ongezeko la madhara kwa mkosaji kulingana na kitabu chetu cha Mwanafunzi-Mzazi Mwongozo wa Maelezo/ Tabia. Ikiwa mzazi anafahamu unyanyasaji shuleni, anapaswa kumpigia simu mwalimu wa mtoto wake, mshauri, mkuu wa kiwango cha darasa, au Simu ya Shule Salama kupitia 889-SALAMA (7233).

### **AFYA NA USALAMA**

Watoto wako wanafaidika na huduma za kitaalamu za muuguzi aliyesajiliwa wakiugua au kujeruhiwa. Wauguzi wetu wako shuleni wakati wote. Utapokea namba za ofisi ya muuguzi kutoka ofisi ya shule.

### **MAGONJWA YA KUAMBUKIZA**

Mtoto wako akipata ugonjwa wa kuambukiza na kukaa nyumbani kwa muda mrefu, kila mwalimu atafanya mipango ya kazi ya muda uliopotea. Kama hauna uhakika lini mtoto wako anapaswa kurudishwa shuleni, mpigie simu muuguzi wa shule au daktari wako.

### **VIGEZO VYA KUTENGWA SHULENI (KUDHIBITI UGONJWA WA KUAMBUKIZA)**

Watoto hutumwa nyumbani kwa sababu zifuatazo:

- 1 Kiwango cha joto cha nyuzi 100F au zaidi
- 2 Kutapika kutokana na ugonjwa
- 3 Kuharisha
- 4 Upele usiotambulika, chawa au ukurutu
- 5 Kushuku maambukizi ya macho
- 6 Kushuku ugonjwa wa kuambukiza

Watoto wanaweza kurudi shuleni kama ifuatavyo:

- 1 Kiwango cha joto chini ya nyuzi 100F kwa masaa 24 bila dawa (k.m., Tylenol, Motrin, nk)
- 2 Upele: hana dalili, na/au cheti kutoka kwa daktari kusema kuwa mwanafunzi haambukizi au matibabu yameanzishwa.
- 3 Kutapika au kuharisha: baada ya lishe ya kawaida kwa masaa 24 - mtoto hatapiki tena au kuharisha.
- 4 Jicho nyekundu: hana dalili, na matibabu kutoka kwa daktari (k.m., matone ya antibiotiki /mafuta ya kupaka) kwa masaa 24 au utambuzi na daktari kwamba mwanafunzi haambukizi.
- 5 Chawa ya kichwa: kuisha kwa chawa, "utitiri" au mayai. Mzazi/mtu mzima lazima aambatane na mtoto kwenye kliniki ili aangaliwe na muuguzi wa shule kabla ya kurudi darasani.

## **DAWA ZA DHARURA**

Maagizo kwa maandishi ya kudumu kutoka kwa daktari wa ushauri wa Wilaya yatapatikana kila mwaka kwa ajili ya usimamizi wa dawa za dharura. Majengo yote yanayokaliwa na wanafunzi katika wilaya hii yana sindano zilizojazwa epinefrini na salfeti majimaji ya kuvuta ya alurterol zinazoweza kupewa na muuguzi wa shule au mfanyakazi mwingine wa shule aliyefunzwa akisimamiwa na muuguzi wakati muuguzi au mfanyakazi aliyefunzwa anaamini, kulingana na mafunzo yake, kwamba mwanafunzi ana mzio unaohatarisha maisha (anaphylactic) au athari ya ugonjwa wa pumu. Wazazi wanastahili kumjulisha muuguzi wa shule au mkuu kama mwanafunzi wao hawezi kupokea albuterol au epinefrini.

## **KUSAMEHEWA KUTOKA KWA ELIMU YA MAZOEZI AU SHUGHULI ZA NJE**

Wanafunzi wanaweza kusamehewa kutoka nje au kutoka kwa madarasa za elimu ya kimwili kwa muda wa siku mbili tu baada ya kupokolewa kwa cheti kutoka kwa mzazi au mlezi. Kumbuka hii lazima ieleze sababu ya msamaha; bainisha tarehe ambazo mtoto anapaswa kusamehewa na, lazima iidhinishwe na mkuu. Kuongeza muda wa kusamehewa kwa ajili ya ugonjwa maalum unaweza kutolewa baada ya kupokelewa kwa maelezo iliyosainiwa na daktari akieleza kuwa: (a) mtoto anapaswa kusamehewa kutoka kwa shughuli za nje na/au elimu ya kimwili, na (b) muda ambao msamaha unatumika.

## **KUFUNZWA NYUMBANI KUTOKANA NA UGONJWA WA MUDA MREFU**

Ikiwa mtoto wako lazima awe nje ya shule kwa muda mrefu, wasiliana na mkuu haraka iwezekanavyo ili iweze kuamuliwa kama mtoto wako anastahili kupata huduma ambazo zitamleta mwalimu nyumbani kwako au hospitalini.

## **UGONJWA AU MAJERAHA**

Ugonjwa au majeraha yakitokea, mtoto atatumizwa kwa muda na muuguzi wa shule au mwanachama wa wafanyakazi wa aliyeidhinishwa. Wafanyakazi wa shule watatoa matibabu ya huduma ya kwanza tu. Ikiwa matibabu ya dharura inahitajika, wazazi watawasiliana. Ikiwa wazazi hawapatikani, mtoto atapelekwa katika chumba cha dharura hospitalini. Kumbuka kwamba nambari ya simu ya dharura ya daktari wa mwanafunzi lazima iwe kwenye faili shuleni.

Kama mtoto anahisi mgonjwa, ana homa, kutapika, au anaharisha wakati wa jioni au asubuhi kabla ya shule, hapaswi kuja shuleni siku hiyo.



## **CHANJO**

Uthibitisho wa chanjo lazima utumwe kwa muuguzi wa shule. Muuguzi ameidhinishwa kukubali nyaraka kutoka kwa daktari kwenye barua ya daktari kwa karatasi rasmi ambayo inajumuisha mwezi, siku, na mwaka wa chanjo kupewa. Wanafunzi wanapaswa kuchanjwa dhidi ya dondakoo, pepopunda, kifaduro, polio, surua, matumbwitumbwi, ukambi, ugonjwa wa ini B and tetewanga (tetemaji). Wanafunzi wa darasa la nane wanatakiwa kuwa na kipimo kimoja cha chanjo ya Tdap na uti wa mgongo. Wanafunzi wa darasa la kumi na mbili wanatakiwa kuwa na vipimo viwili vya chanjo ya uti wa mgongo. Wanafunzi ambao hawana kinga ya kutosha au hawana nyaraka za msamaha hawataruhusiwa kuhudhuria darasa. Kliniki ya shule ina taarifa zinazohusu mahitaji ya chanjo.

Maeneo ya Idara za Afya za Kaunti ya St. Louis ambapo chanjo zinapatikana zinaweza kuchukuliwa kutoka kwa kliniki ya shule.

## **TAARIFA ZA MATIBABU**

Lazima tuwe na TAARIFA za MATIBABU ya mtoto wako kwenye faili. Ofisi ya mapokezi ya shule inapaswa kuwa na nambari ambapo unaweza kufikiwa ikiwa ugonjwa au dharura. Inapaswa pia kuorodhesha mtu ambaye anapatikana kila wakati kuchukua mtoto wako ikiwa hatuwezi kukufikia.

Sasisha maelezo ya dharura ya mtoto wako wakati wowote mabadiliko yanapohitajika katika majina na/au namba za simu.

## **TATHMINI YA AFYA YA AKILI NA HUDUMA ZA USHAURI NASAHA**

Wanafunzi wakati mwingine wanaweza kuhitaji ushauri ili kutatua masuala mbalimbali za kihisia. Ikiwa ushauri wa nje unahitajika, tafadhali wasiliana na mshauri/mfanyakazi wa kijamii wa shule yako kwa rufaa ya mashirika yafuatayo:

- Family Solutions for Kids (K-12)
- Safe Connections (9-12)
- Lutheran Family and Children's Services (K-12)
- Children's Foundation of Mid-America (K-12)
- Community Psychological Service (K-12)
- Children's Home Society kupitia kwa Wilaya Maalum ya Shule (K-12)
- DePaul SSM Behavioral Health Services (K-12)
- National Alliance on Mental Illness (K-12)

## **UCHUNGUZI WA KIMWILI**

Inapendekezwa kwamba kila mtoto anayehudhuria Wilaya ya Shule ya Hazelwood anapaswa kufanya uchunguzi kamili wa kimwili mwanzoni mwa mwaka wa shule katika shule ya chekechea, madarasa za 4, 7 na 10. Inapendekezwa pia kwamba wanafunzi wapya kwenye mfumo wa shule wanapaswa kufanya uchunguzi kamili wa kimwili bila kujali kiwango cha darasa. Fomu za kusudi hili zinapatikana kutoka kwa muuguzi wa shule au kwenye tovuti ya Huduma za Afya.

## **TARATIBU ZA KUSIMAMIA DAWA ZA WANAFUNZI KWA WANAOHITAJI DAWA SHULENI**

Sera ya Wilaya ya Hazelwood School (JHCD) inaruhusu kupeana dawa kwa wanafunzi wanaoitaka wakiwa shuleni ili kuwawezesha kubaki shuleni na kushiriki katika masomo yao. Zifuatazo ni taratibu zinazohitajika za kutoa huduma hii kwa wanafunzi.

- Wilaya itakubali lebo ya maagizo kama sawa na agizo la daktari au agizo la daktari kwa ajili ya dawa. Fomu iliyokamilishwa ya ruhusa ya wazazi inahitajika pia. Mwelekeo ulioandikwa ni pamoja na jina la mwanafunzi, jina la dawa, kipimo, mirudio ya kupewa, saa ya dawa ni kupewa shuleni, sababu ya dawa, madhara yanayowezezana na tarehe ya kusimamisha huduma ya dawa kupewa. (Fomu inapatikana katika kliniki.)
- Dawa lazima yafikishwe na mzazi/mlezi au mtu mwingine mzima mwenye jukumu.
- Hakuna dawa inayonunuliwa bila agizo la daktari itapeanwa kwa mwanafunzi bila fomu ya ruhusa ya wazazi iliyokamilishwa.
- Wilaya **haitaweza** kupeana kipimo cha kwanza cha dawa yoyote.
- Mzazi/mlezi wa mwanafunzi lazima achukue jukumu la kumjulisha muuguzi juu ya mabadiliko yoyote katika afya ya mwanafunzi au dawa.
- Ikiwa kuna mabadiliko katika dawa au kipimo cha dawa, agizo iliyoandikwa inahitajika kutoka kwa daktari.
- Dawa zote we kwa chupa ya maagizo ya mwanzo, au chombo cha mwanzo ya kununua bila agizo la daktari, na isizidi dawa za siku 30 na taarifa zifuatazo kwenye lebo:
  - Jina la mtoto
  - Jina ya dawa na kipimo
  - Jina la Daktari
  - Jinsi dawa inavyopaswa kutolewa (wakati na marudio)
  - Mahitaji maalum ya kuhifadhi (k.m. kuwekwa kwenye friji)
- Ratiba ya II dawa za (dutu zilizodhibitiwa) zitahesabiwa baada tu ya kupokelewa, kwa kutumia fomu inayopatikana katika kliniki.
- Sera pia inashughulikia haja ya wanafunzi wenye ugonjwa sugu wa kupumua, ambao hutumia dawa ya kuvuta yanayopimwa kwa mita, kutumia dawa zao shuleni.
- Wazazi/walezi wana jukumu la kuchukua dawa yoyote ambayo yanabaki mwishoni mwa mwaka wa shule. Kama hayatachukuliwa, muuguzi ataharibu kile kilichobaki.

Wazazi ambao wana maswali au wasiwasi wanapaswa kuwasiliana na muuguzi wa shule.

Hakuna mwanafunzi anayeruhusiwa kuwa na dawa ya aina yoyote (hata matone ya kikohozi, aspirini, nk.) katika milki yake. Utaratibu wa daktari unahitajika kwa wanafunzi wenye dawa ya kuvuta au insulini kutumia dawa mwenyewe. Tafadhali wasiliana na muuguzi wako wa shule kwa maelezo zaidi. Dawa zingine zote lazima ziwekwe katika ofisi ya muuguzi. Dawa husimamiwa katika kliniki tu na wafanyakazi wa shule wenye ujuzi. Nafasi ya friji unapatikana.

## **MAHITAJI MAALUM YA MATIBABU**

Ni muhimu tujue kama mtoto wako ana mahitaji maalum ya kiafya. Ni wajibu wa mzazi/mlezi kujaza fomu sahihi za dharura na kutupatia taratibu za dharura katika tukio ambalo mtoto wako anahitaji kutibiwa kwa hali kama hiyo ya dharura kama mzio au matokea ya kisukari.

## **SERA YA KITAMBULISHO (SHULE ZA KATI NA SEKONDARI TU)**

Wanafunzi wote lazima wavae kitambulisho chao kilichotolewa na shule wakati wa masaa ya shule. Vitambulisho vya wanafunzi lazima vivaliwe kwenye lkamba iliyotolewa na shule shingoni wakati wa masaa ya shule. Vitambulisho lazima vivaliwe mbele na lazima vionekane wakati wote. Wanafunzi hawatachafua vitambulisho vyao (kuandika kwenye kitambulisho, kuweka vibandiko kwenye kitambulisho, nk). Wanafunzi lazima waonyeshe kitambulisho chao kwa mtu mzima yeyote anapombwa.

### **IKIWA KUNA SUALA SHULENI**

Wilaya ya Shule ya Hazelwood imejitolea kwa mafanikionikiwa ya kila mwanafunzi. Inaeleweka vyema kuwa matokeo bora yanapatikana wakati kazi ya nyumbani na shule yanatimizwa kwa ushirikiano. Ingawa hatua zinachukuliwa ili kuhakikisha kuwa kila mwanafunzi ana uzoefu mzuri wa shule, masuala wakati mwingine yatatokea. Ili kuhakikisha kuwa masuala yanashughulikiwa mara moja na kwa ufanisi, Wilaya imetayarisha miongozo ya kutafuta suluhisho ya masuala:

1. Ongea kwanza na mwalimu kama suala hilo linahusiana na darasa.
2. Unaweza kuwasiliana na mkuu wa kiwango cha darasa ikiwa unapenda kupokea msaada katika kutatua masuala ambayo hayatatuliwi baada ya kuzungumza na mwalimu.
3. Unaweza kuwasiliana na mkuu wa shule ikiwa unapenda kupokea msaada katika kutatua masuala ambayo hayatatuliwi baada ya kuzungumza na mkuu wa kiwango cha darasa au ikiwa yanahusisha jambo la shule. Maswali yanayohusiana na Wilaya Maalum ya Shule yataelekezwa kwa mratibu wa eneo hilo.
4. Unaweza kuwasiliana na msaidizi wa mrakibu ikiwa unapenda kupokea msaada katika kutatua masuala ambayo hayatatuliwi baada ya kuzungumza na mkuu wa shule. Masuala mengine au maswali yanayohusu wilaya ya shule yanapaswa kuelekezwa kwa Msimamizi anayefaa katika Ofisi Kuu.
5. Unaweza kuwasiliana na naibu mrakibu kupokea msaada katika kutatua masuala ambayo hayajatatuliwa baada ya kuzungumza na msaidizi wa mrakibu.
6. Unaweza kuwasiliana na msimamizi (kwa maandishi) ikiwa unataka kupokea msaada katika kutatua masuala ambayo hayatatuliwi baada ya kuzungumza na naibu mkuu.

### **MATUMIZI YA MTANDAO**

Mtandao unapatikana kwa matumizi ya utafiti. Tutafuata Sera ya Matumizi Inayokubalika ya Wilaya ya Hazelwood. Maktaba na madarasa vitakuwa na ufikiaji wa Tovuti ya Ulimwengu Mzima kupitia Mtandao. Wanafunzi hawataruhusiwa kuunda, kutuma au kupokea barua pepe shuleni isipokuwa kazi ni sehemu ya mradi wa masomo ulioidhinishwa. Fursa ya kutumia mtandao inaweza kufutwa kwa sababu ya matumizi yasiyofaa ya fursa ya ufikiaji. Mwanafunzi yeyote kwenye sehemu isiyofaa atapoteza leseni yake zikwa mwaka mmoja wa shule. "Wanafunzi hasa wanakubali kutowasilisha, kuchapisha, au kuonyesha uharibifu wowote, usio sahihi, unyanyasaji, machafuko, hasira, mwelekeo wa kijinsia, kutisha, ubaguzi wa rangi, au nyenzo haramu, wala mwanachama kuhimiza matumizi ya vitu vinavyodhibitiwa." Wanafunzi hawawezi kutuma, kuchapisha, au kupakua faili zozote bila idhini ya mwalimu anayesimamia. Kufanya hivyo kunaweza kusababisha upotevu wa fursa ya mtandao. Mwanafunzi yeyote anayepata shida kupata tovuti kwa sababu za kielimu anapaswa kuwasiliana na mwalimu.

## **KUONDOKA CHUONI**

Wanafunzi hawaruhusiwi kuondoka chuoni isipokuwa ruhusa iliyoandikwa kutoka kwa wazazi imetolewa na kuidhinishwa ofisini. Wanafunzi wanaotaka au wanaohitaji kutembea nyumbani lazima wawe na cheti kwenye faili ofisini ya ruhusa kutoka kwa mzazi/walezi kwa mwanafunzi kutembea nyumbani.

Usafiri wa mabasi hutolewa siku za kuondoka mapema mapema, lakini wanafunzi wataruhusiwa kutembea ikiwa wana kijikaratas cha i ruhusa kutoka kwa wazazi iliopo kwa faili ofisini kabla ya siku ya kuondoka mapema. Ikiwa ufafanuzi zaidi unahitajika, tafadhali wasiliana na utawala wa jengo.

## **TARATIBU YA MAKTABA**

Maktaba ya Shule ina vitabu vya majalada magumu na mepesi kwa matumizi ya wanafunzi wetu na kitivo. Maktaba iko wazi masaa za kawaida za kwa matumizi ya wanafunzi na hutumiwa mara kwa mara na madarasa zinazofanya utafiti na / au kuazima. Madhumuni ya maktaba ya shule ni kutoa rasilimali za elimu kwa wanafunzi wote. Maktaba pia ni mahali pa kupumzika na starehe ya kusoma, pamoja na mahali pa mafunzo na utafiti kwa utulivu. Ili kudumisha mazingira haya, tabia sahihi ya maktaba inatarajiwa.

## **MAKABATI**

Kila mwanafunzi wa shule ya kati na sekondari atapewa kabati lake na kufuli ukumbini mwanzoni mwa mwaka wa shule. Vifuli vya binafsi haviwezi kutumika kwenye ukumbi wa makabati. Makabati yote ni ardhi na majengo ya Wilaya ya Shule ya Hazelwood na yanaweza kuingiwa kwa hiari ya utawala.

- Makabati LAZIMA yafungwe wakati wote. Kuacha kabati iliyowekwa kwenye nambari hufanya iweze kufikiwa na wanafunzi wengine.
- Nambari za kufunga kabati LAZIMA ISI shirikiswe au kubadilishwa na wengine.
- Wanafunzi wanaobadili makabati bila ruhusa kutoka kwa ofisi au kutumia kabati ya mwanafunzi mwingine, watakabiliwa na hatua za kiadhibi.
- Wanafunzi wanawajibika kwa vitu vyote vilivyowekwa katika kabati lao.

Kwa kuwa kabati ni mali ya shule, inaweza kukaguliwa. Wanafunzi lazima watumie kabati ambayo imepangiwa kwao tu. Ili kuhakikishia kuwa vifaa katika jengo letu vinatumia kwa uangalifu, vibandiko au vitu vilivyowekwa mkanda haviwezi kutumika juu au ndani ya makabati. Ukubwa wa makabati yetu yanahitaji kuwekwa vifaa vya shule vinavyohitajika, vitabu, na kanzu pekee. Kufuli ikipotea, kufuli mpya itatolewa kwa ada ya kubadilisha ya \$5.00.

## **MOCAP KATIKA WILAYA YA SHULE YA HAZELWOOD**

Kuanzia Januari 2019, mwanafunzi yeyote katika Chekechea had darasa la 12 aliyejiandikisha katika Wilaya ya Shule ya Hazelwood na ambaye pia alijiandikishwa kama mwanafunzi wa kila siku muhula uliopita anaweza kuchagua kuchukua kozi mtandaoni kupitia mtoa huduma anayependelewa na Wilaya, **Launch**, au kupitia kwa Programu ya Ufikiaji wa Kozi ya Missouri (**Missouri Course Access Program (MOCAP)**) iliyoandaliwa kupitia kwa Idara ya Elimu ya Msingi na Sekondari ya Missouri (**Department of Elementary and Secondary Education (DESE)**). Ili kupata maelezo zaidi, tembelea ukurasa wa Idara ya Mtaala na Mafundisho kwenye wavuti ya wilaya.

## **TARATIBU ZA MAEGESHO (SHULE YA SEKONDARI)**

Maegesho yamehifadhiwa kwa ajili ya kitivo, wafanyakazi, wazazi, na wageni. Wanafunzi tu ambao wana pasi maegesho yalitolea na ofisi ambayo ina mwonekano nzuri anaweza kuegesha chuoni. Wanafunzi wanapaswa kuegesha katika maeneo yaliyotengwa.

Ili kila mtu awe salama wakati wa masaa ya shule, madereva wanaombwa kuheshimu alama zote za kasi trafiki, ishara za kushukisha na kuchukua na kutumia heshima ya kawaida wanapoendesha gari kwenye majengo ya shule. Tafadhali angalia maafisa wote wa usalama wa shule, maafisa wa rasilimali za shule, na alama kwenye chuo cha shule.

### **VITAFUNIO/VYAKUFURAHISHA VYA KARAMU (SHULE YA MSINGI)**

Wilaya ya Shule ya Hazelwood inafua mapendekezo ya Idara ya Afya ya Kaunti ya St. Louis na Miongozo ya Advanced Missouri Eat Smart kuhusiana na vitafuno vya karamu. Chakula kilichopikwa katika nyumba za watu binafsi hakiruhusiwi. Wilaya ina mpango mpya ya vitafuno kwa karamu darasani za siku ya kuzaliwa. Wazazi au walezi wanaotaka kupanga siku ya kuzaliwa ya mtoto wao shuleni wanahimizwa kukamilisha fomu ya kuagiza kutoka kwa Idara ya Lishe ya Mtoto.

Vitafuno vinavyopatikana vinazingatia Miongozo ya Eat Smart Advanced yalioombwa na Wilaya na barafu na juisi hayana visababisha mzio. Vitafuno vyovyoyote vinavyoletwa ndani kutoka nje kwa ajili ya karamu darasani ya siku ya kuzaliwa, lazima yawe yamepakiwa mapema, yanafuata Miongozo ya Eat Smart na yanahitaji kuidhinishwa na mwalimu na/au muuguzi wa shule ili kuhakikisha kuwa hayana visababisha mzio.

Vitambaa, masahani, vyombo vya kulia, na vitafuno yatawasilishwa kwa mwanafunzi na wanafunzi wenzake katika kipindi chao cha chakula cha mchana. Wanafunzi wa shule ya utotoni watapokea vitafuno vyao darasani.

Ikiwa una maswali kuhusu mpango wa karamu ya darasani ya siku ya kuzaliwa, wasiliana na Idara ya Lishe ya Mtoto wa Shule ya Hazelwood katika (314) 953-5990 au wasiliana na mkahawa wa shule ya mtoto wako.

Kwa kawaida, kuna karamu mbili ya darasa kwa mwaka. Kila mkuu wa shule na wafanyakazi wataamua ni karamu gani zinafaa kwa shule zao. Miongozo ya Advanced Missouri Eat Smart yanahitaji chakula ambacho kinakidhi miongozo fulani ya afya. Kwa hiyo, keki ndogondogo na peremende haziruhusiwi. Nenda kwenye tovuti ya Wilaya ili uone Miongozo ya Eat Smart.

### **MAKAZI**

Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na makao au kuishi muda wote katika Wilaya ya Shule ya Hazelwood isipokuwa vinginevyo ana haki ya kisheria kuhudhuria wilaya hii. Hii itaamuliwa na Ofisi ya Makazi. Wilaya inaweza kuomba sasisho kuhusu makazi wakati wowote. Ikiwa ya kukodisha, makubaliano ya wakati huu yataombwa kila mwaka ili kuhakikisha mahudhurio yasiyokatishwa.

Ikiwa unashuku mtu anakiuka mahitaji ya makazi, tafadhali ripoti hayo kwa Ofisi ya Makazi kwa 314-953-5041.

## **USALAMA NA AMANI**

### **SIMU YA MOJA KWA MOJA YA SHULE SALAMA**

Wanafunzi na wazazi sawa wanahimizwa kuripoti tishio lolote dhidi ya mwanafunzi, kitivo, wafanyakazi au mjengo kwa mkuu anayesimamia, hata hivyo, ripoti isiyojulikana inaweza kuchukuliwa kupitia kwa Simu ya Moja-kwa-Moja ya Shule Salama katika **314-889-SAFE (7233)**.

### **KUOMBAOMBA**

Wanafunzi hawawezi kuuza vitu shuleni, isipokuwa kama uuzaji umeidhinishwa na Mkurugenzi wa Shughuli za shule na ni shughuli ya kuchangisha fedha kwa ajili ya shughuli au klabu inayofadhiliwa na shule.

### **PROGRAMU MAALUM**

Wilaya ya Shule ya Hazelwood inatoa huduma kwa wanafunzi na wazazi wao kuanzia kuzaliwa hadi miaka 21. Zifuatazo ni baadhi ya programu hizo. Piga simu kwa maelezo zaidi.

Programu ya Elimu ya Utotoni wa Mapema kwa wanafunzi wa miaka mitatu na minne – 953-7650  
Elimu Maalum ya Utotoni kwa wanafunzi wa miaka mitatu na minne - 953-4957  
Wasomi wa Lugha ya Kiiingereza - 953-4954

Gifted Alternative Learning (GALACTIC) Shughuli Zinzohusiana na Watoto - Programu ya wanafunzi wenye vipaji na wenye talanta inapatikana kwa wanafunzi wanaostahili - 953-4954

Programu ya Wazazi kama Walimu (PAT) inatoa uchunguzi, madarasa ya mzazi / mtoto, mikutano ya kikundi na ziara za kibinafsi za nyumbani - 953-7635

### **HUDUMA MAALUM ZA ELIMU HUTOLEWA NA WAFANYAKAZI MAALUM WA WILAYA YA SHULE**

Programu maalum za elimu hutolewa kwa wanafunzi wanaostahili kulingana na vigezo vilivyozanzishwa na Wilaya Maalum ya Shule, kwa mujibu wa miongozo ya serikali. Wanafunzi walio na matatizo za kuona, mifupa, uharibifu wa kusikia, na wanafunzi wengine wenye uharibifu mwingine wa kiafya wanapata huduma kulingana na miongozo ziliyoanzishwa na Jimbo la Missouri na Wilaya Maalum ya Shule.

### **VITABU VYA KIADA**

Vitabu vyote vya kiada vinapeanwa kwa wanafunzi; hata hivyo, malipo lazima yafanywe kwa vitabu vilivyopotea au vilivyoharibika. Wanafunzi wanapaswa kuweka jina lao katika mafungu yote kutumia wino. Faini zitapimwa kwa vitabu vilivyopotea au vilivyoharibika.

### **NAKALA**

Maombi yote ya nakala lazima yafanywe kwa maandishi kwa msajili wa shule. Fomu za maombi ya nakala zinapatikana katika ofisi ya msajili wa shule. Kila mwanafunzi aliyeandikishwa kwa sasa anaweza kuomba nakala tatu bila gharama yoyote; kila ombi la ziada la nakala litachapishwa kwa ada ya kawaida.

## **WATU WA KUJITOLEA**

Wilaya ya Shule ya Hazelwood inathamini masaa yasiyohesabika ambayo wafanyakazi wetu wa kujitolea wa metumia kuboresha ubora wa elimu kwa wanafunzi wetu. Wafanyakazi wa kujitolea wa shule ni sehemu muhimu ya mafanikio ya wilaya yetu ya shule. Wafanyakazi wote wa kujitolea wa shule wanatakiwa kukamilisha maombi na makubaliano ya kujitolea, pamoja na kusaini makubaliano ya usiri, makubaliano ya matumizi ya teknolojia, na taarifa ya tahadhari za kila kitu.

Kwa kuongezea, uchunguzi wa nyuma utafanywa kwa kila mtu alinayejitolea ambaye ana mawasiliano ya kuendelea na mara kwa mara na mwanafunzi, asiyesimamiwa au mmoja-kwa-moja na wanafunzi, anakua na wanafunzi, anahudhuria safari za masomo ya nje au kutumikia katika jukumu la usimamizi. Kuna viwango viwili vya kujitolea: Wafanyakazi wa Kujitolea wa kawaida na wanaoidhinishwa kwa Mandharinyuma ya Alama za Vidole na kila mmoja ana mchakato wa kipekee wa uchunguzi.

### **Kiwango Cha Kawaida Cha Kujitolea**

**Kiwango cha kawaida kinakupa nafasi ya kujitolea kwa shughuli za Wilaya zinazoundwa kwa mazingira ya kikundi kikubwa.**

### **Jinsi ya Kuomba**

- Wafanyakazi **wote** wa kujitolea wanahitaji kujiandikisha na Rasilimali za Wafanyakazi kwa kubonyeza kiungo: <http://bit.ly/2OEARMf>
- [Kamilisha kifurushi cha kujitolea kilicho kwenye tovuti ya HSD](#)

### **Usajili na Upangaji**

**Piga simu:** Idara ya Afya na Huduma za Wazee wa Missouri kwa **866.422.6872**

Thibitisha ikiwa tayari uko kwenye Usajili wa Huduma ya Familia ya Missouri. Kama umeorodheshwa, omba barua ya uthibitisho iliyosasisiwa.

Kama kwa sasa hauko kwenye rejista, tembelea [www.health.mo.gov/safety/fcsr](http://www.health.mo.gov/safety/fcsr) kujiandikisha mtandaoni au kamilisha fomu ya Usajili wa Watumishi iliyopo katika Pakiti ya Kujitolea kwenye tovuti ya Wilaya.

### **Malipo**

Ada ya **wakati-mmoja** ni:

\$15.25 mtandaoni, Kadi ya Mkopo au Kadi ya Makato (mgeuko wa wiki 2)

\$14 kupitia Posta ya Marekani, Cheki kulipwa kwa MDHSS, jumuisha nakala ya kadi ya social security (mgeuko wa wiki 8) Tuma kwa: MDHSS-Fee Receipts, P.O. Box 570, Jefferson City, MO 65102

### **Wafanyakazi wa Kujitolea Walioidhinishwa kwa Mandharinyuma ya Alama za Vidole**

**Wafanyakazi wa kujitolea ambao alama za vidole vilichukuliwa wanaweza kuachwa peke yao na wanafunzi kwa kipindi.**

Muswada wa Missouri House 604, kifungu cha 168.188 kinalazimu mtu yeyote anayejitolea ambaye anaweza kuachwa kwa kipindi peke yake na mwanafunzi kufanyiwa ukaguzi wa mandharinyuma ya alama za vidole na Doria ya Barabara kuu ya Missouri.

## **Jinsi ya Kuomba**

- Wafanyakazi **wote** wa kujitolea wanahitaji kujiandikisha na Rasilimali za Wafanyakazi kwa kubonyeza kiungo: <http://bit.ly/2OEARMf>
- Kamilisha kifurushi cha kujitolea kilicho kwenye tovuti ya HSD. Ikiwa uliishakamailisha pakiti ya kujitolea, hamna haja ya kukamilisha mpya.

## **Usajili wa Kuchukuliwa Alama za Vidole na Upangaji**

Mtandaoni: Tovuti ya Historia ya Jinai ya Missouri Inayojiendesha [WWW.MACHS.MO.GOV](http://WWW.MACHS.MO.GOV)

Simu: **844.543.9712**

Nambari ya Hazelwood #**1825 (Kwa Wabadala/Kujitolea)**

Muhimu kurekodi #Kitambulisho cha uthibitisho wa Uandikishaji wa Universal, utahitaji #**UEID** ili kupata alama za vidole.

## **Malipo**

Ada ya **wakati-mmoja** ni \$41.75

Hakuna malipo yanayokubaliwa mtandaoni. Malipo yanakusanywa wakati wa uchukuaji wa alama za vidole.

**HAKUNA PESA TASLIMU** au Cheki wa Kibinafsi. Kadi ya Mkopo, Kadi ya Makato, Cheki ya Kibiashara au Utaratibu wa Pesa.

## **Aina za Vitambulisho Vinavyokubalika**


Ili kupata alama za vidole, lazima uwasilishe kitambulisho **halali** kilicho na picha kilichotolewa na serikali kama vile Leseni ya Madereva, Kitambulisho cha Jimbo, Pasipoti au Kitambulisho cha Wanajeshi. Nakala na kitambulisho kilichokwisha muda wake hazitakubaliwa.

## **Taarifa na Beji**

Rasilimali ya Wafanyakazi (HR) itawajulisha wafanyakazi wa kujitolea, kwa maandishi, ikiwa imeidhinishwa au kukataliwa. Ikiwa imeidhinishwa, njoo kwa HR ili upate beji yako mpya.

Leta pakiti yako ya kujitolea. Beji hutengenezwa kila siku kati ya 2:00 asubuhi - 6:00 mchana.



Hazelwood  
School   
District

*"A Culture of High Expectations and Excellence!"*  
Utamaduni wa Matarajio makubwa na Ubora"

# Matetemeko ya Ardhi Missouri

Hatari ya juu ya tetemeko la ardhi nchini Marekani nje ya Pwani ya Magharibi iko katika **Zoni ya New Madrid Seismic** katikati ya Mustatili ya Missouri kusini-mashariki. Uharibifu wa matetemeko ya ardhi sio mara kwa mara kama huko California, lakini yanapotokea, uharibifu hapa unaweza kufunika eneo zaidi ya mara 20 zaidi ya tukio kama hilo huko kutokana na asili ya vifaa vya kijiolojia katika eneo hili. Tetemeko kubwa la ardhi linaweza kumaanisha janga la uharibifu katika maeneo ya St. Louis na kusini-mashariki mwa jimbo, na uharibifu mkubwa Missouri kote.

**Zoni ya New Madrid Seismic na eneo jirani katikati ya Marekani wanapata watan wa matetemeko ya ardhi zaidi ya 200 kwa mwaka.** Mengi hayawawezi kuhisiwa, lakini chache yanaweza kusababisha uharibifu wa kupimika.



Wataalamu wanasema kwamba kuna nafasi ya **asilimia 25 hadi 40 kwa tetemeko kubwa la ardhi** kwa kipindi cha miaka 50. Matokeo yake yanaweza kuwa uharibifu mkubwa kutoka St. Louis hadi Memphis. Tetemeko kubwa la mwisho katika Zoni ya New Madrid Seismic lilikuwa katikati ya kusini-mashariki mwa Missouri, karibu na mji wa Charleston, mwaka 1895.

**Matetemeko Makubwa ya New Madrid ya 1811-12** yalikuwa makubwa zaidi katika historia ya Marekani mashariki mwa Milima ya Rocky. Matetemeko kubwa yaliharibu makao, yaliunda maziwa na kwa muda mfupi kugeuza mtiririko wa Mto wa Mississippi. Matetemeko ulihisiwa mbali mpaka pwani ya mashariki.

*Imetayarishwa kulingana na Sheria za Missouri Zilizorekebishwa, Sura ya 160, Sehemu ya 160.455*

Shirika la Usimamizi wa Dharura la Jimbo la Missouri  
PO Box 116, Jefferson City, Missouri 65102  
Simu: 573/526-9100 Faksi: 573/634-7966  
Barua pepe: [mosema@sema.dps.mo.gov](mailto:mosema@sema.dps.mo.gov)



# Hifadhi Ukurasa Huu!

*Ili kusaidia familia yako kunusurika tetemeko la ardhi, fahamu nini cha kufanya KABLA, WAKATI, na BAADA ya tetemeko kubwa kupiga.*

## KABLA:

- ✓ Weka pamoja mkoba wa dharura – tochi, vifaa vya huduma ya kwanza, redio, maji ya kunywa, blanketi
- ✓ Fanya mpango wa mawasiliano ya familia - tafuta jamaa anayeishi angalau maili 100 mbali ambaye kila mtu anaweza kupigia simu "kujisali" kwake kuwaambia familia kuwa uko salama
- ✓ Hakikisha kuwa vitu vyote vizito au vinavyoweza kuvunjika viko kwenye rafu za chini
- ✓ Fahamu jinsi ya kuzima matumizi

## UNAPOTENDEKA:



- ✓ JIANGUSHE chini kwa sakafu
- ✓ JIFUNIKE chini ya meza au dawati imara, na kufunika uso wako na kichwa kwa mikono yako
- ✓ SHIKILIA kitu imara mpaka mtetemeko yakome
- ✓ Ikiwa unaendesha gari, toka barabarani, mbali na majengo na miti za umeme au simu, na ukae kwenye gari lako
- ✓ Ukiwa nje, jiangushe chini, mbali na vitu vikubwa, na ufunike uso na kichwa chako na mikono yako

## BAADAYE:

- ✓ Tafuta familia yako; chunguza majeraha
- ✓ Ikiwa ni lazima, piga simu 911 kupata msaada
- ✓ Ukinusa gesi au kusikia mlio wa sss, nenda nje - zima vali ya gesi
- ✓ Kuwa mwangalifu ili kuepuka waya za umeme na vioo vilivyovunjika
- ✓ Sikiza habari za hivi karibuni za dharura
- ✓ Kuwa tayari kwa mishutuko ya baadaye

Shirika la Usimamizi wa Dharura la Jimbo la Missouri

PO Box 116, Jefferson City, Missouri 65102

Simu: 573/526-9100 Faksi: 573/634-7966

Barua pepe: [mosema@sema.dps.mo.gov](mailto:mosema@sema.dps.mo.gov)



Mpendwa Mzazi au Mlezi:

Wilaya yetu inatakiwa kukujulisha juu ya habari kuwa, kwa mujibu wa Sheria ya Kila Mwanafunzi Anafanikiwa ya mwaka 2015 (Sheria ya Umma 114-95), una haki ya kujua.

Baada ya ombi lako, wilaya yetu inahitajika kukupatia kwa wakati unaofaa, taarifa zifuatazo:

- Ikiwa mwalimu wa mwanafunzi wako ametimiza vigezo vya Serikali vya kustahili na leseni kwa ngazi za darasa na maeneo ya masomo ambamo mwalimu hutoa maelekezo.
- Ikiwa mwalimu wa mwanafunzi wako anafundisha chini ya hali ya dharura au hali nyingine ya utoaji wa muda ambayo vigezo vya Serikali vya kustahili na leseni vimeondolewa.
- Ikiwa mwalimu wa mwanafunzi wako anafundisha katika nyanja ya nidhamu ya dhibitisho ya mwalimu.
- Ikiwa mtoto wako anapatiwa huduma na waisadizi wa maelekezo na, ikiwa ni hivyo, kushtahili kwao.
- Mbali na taarifa ambazo wazazi wanaweza kuomba, jengo linalopokea fedha za Kichwa I.A lazima zitoe kwa kila mzazi binafsi:
